## YALIYOMO


1.0 Utangulizi ........ 4
1.1 Idadi ya Watu ........ 4
2.0 Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita Kisekta ........ 5
2.1 Mpango na Bajeti ya Mkoa na Halmashauri ........ 6
2.2 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ........ 10
2.2.1 Mafanikio ........ 10
2.3 Sekta ya Elimu ........ 12
2.3.1 Elimu ya Msingi ........ 12
2.3.2 Elimu ya Sekondari ........ 15
2.3.3 Chuo Kikuu cha Dodoma ........ 17
2.3.3.1 Mafanikio ........ 17
2.3.4 Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ........ 19
2.3.4.1 Taaluma ........ 19
2.3.4.2 Utawala ........ 20
2.3.4.3 Maendeleo ya Miundombinu ........ 22
2.3.4.4 Miradi iliyotekelezwa kwa kutumia Fedha za Ruzuku ........ 23
2.3.4.5 Miradi iliyotekelezwa kwa kutumia Mapato ya Ndani ya Chuo 24
2.3.4.6 Huduma Ushauri Uelekezi ........ 25
2.3.4.7 Miradi ........ 26
2.3.4.8 Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET) ........ 27
2.3.5 Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) ........ 27
2.4 Sekta ya Afya ........ 28
2.4.1 Hospiatli ya Rufaa ya Mkoa ........ 36
2.4.2 Hospitali ya Benjamin Mkapa ........ 40
2.4.3 Huduma zinazotolewa na Hospitali ........ 40
2.4.4 Mapato ........ 41

2.4.4.1 Mapato kutoka Serikali Kuu - 30,488,380,926.81 ........................ 41
2.4.4.2 Mapato ya ndani Shilingi 43,366,164,099.75 ............................... 42
2.4.5 Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ............................ 44
2.5 Sekta ya Maji ........................................................................ 48
2.5.1 DUWASA .............................................................................. 48
2.5.2 RUWASA .............................................................................. 50
2.6 Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ............................. 51
2.6.1 TANROADS .......................................................................... 51
2.6.2 TARURA ............................................................................... 62
2.6.3 LATRA .................................................................................. 64
2.6.3.1 Usafiri wa ndani ya Mkoa ................................................ 64
2.6.3.2 Usafiri wa Magari ya masafa marefu. .................................. 65
2.6.3.3 Udhibiti na Kupunguza ajali. .............................................. 66
2.6.4 Mawasiliano ya Simu za Mkononi ........................................... 67
2.6.4.1 Huduma za Matangazo kwa Njia ya Redio ............................. 68
2.6.4.2 Huduma za Televisheni ...................................................... 69
2.6.4.3 Huduma za Matangazo ya TV kwa Njia ya Waya .................... 69
2.6.4.4 Huduma ya TV kwa Njia ya Miundombinu Iliyosimikwa Ardhini (DTT) ........................................................................ 70
2.6.4.5 Huduma ya TV kwa Njia ya Satelaiti ..................................... 70
2.7 Sekta ya Kilimo, Mifugo na Ushirika ......................................... 71
2.7.1.1 Ruzuku za Pembejeo za Kilimo ............................................ 74
2.7.2 Sekta ya Mifugo ..................................................................... 77
2.8 UWEKEZAJI VIWANDA NA BIASHARA ................................. 80
2.9 Shirika la Nyumba la Taifa Mkoa wa Dodoma. ........................ 84
2.9.1 Mafanio ya Shirika la Nyumba(NHC) Mkoa wa Dodoma ...... 84
2.10 Wakala Wa Majengo Tanzania (TBA) Utangulizi .................... 85
2.10.1 Miradi Inayotekelezwa Dodoma ............................................. 86
2.10.1.1 Miradi ya Kimkakati ......................................................... 86

2.10.1.2 Miradi ya Ushauri ........................................................................ 89
2.11 Sekta ya Nishati na Umeme ........................................................ 91
2.11.1 TANESCO ...................................................................................... 91
2.12 Wakala wa Vipimo (WMA) .......................................................... 97
2.13 TANAPA ........................................................................................ 98
2.14 Mafanikio Yaliyopatikana Katika Utalii .................................... 98
2.15 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ........................................................ 102
2.15.1 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ............................... 102
**3.0** MIPANGO YA MKOA KWA MWAKA 2023/24-2025/26 ... 103
3.1 Malengo ya Ukusanyaji Mapato ya Halmashauri ................... 103
3.2 Malengo ya Seksheni ya Elimu .................................................. 104
3.3 Malengo yaliyowekwa kwa ajili ya kuimarisha sekta ya Afya mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ............................................................ 104
3.4 Malengo ya Sekta ya Kilimo ....................................................... 106
3.5 Malengo ya Sekta ya Mifugo ...................................................... 106
3.6 Malengo ya Sekta ya Maliasili na Utalii .................................... 107
3.7 Malengo ya Sekta ya Viwanda ................................................... 108
3.8 Malengoya Sekta ya Ushirika ..................................................... 108
3.9 Malengo TANROADS mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ........ 108
3.10 Malengo TARURA mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ............. 109
3.11 Lengo Uwanja wa Ndege mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 109
3.12 Malengo Sekta ya Maji mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ...... 109
3.13 Malengo RUWASA mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ............ 110
3.14 Malengo TANESCO mwaka 2022/2023 hadi 2025/26 ........... 110
3.15 Malengo Sekta ya TEHAMA ...................................................... 110

## 1.0 Utangulizi

Mkoa wa Dodoma una Wilaya **07** (Bahi, Chamwino, Chemba, Dodoma, Kondoa, Kongwa na Mpwapwa) na Halmashauri **08** ambazo ni Bahi, Chamwino, Chemba, Dodoma Jiji, Kondoa, Kondoa Mji, Kongwa na Mpwapwa. Aidha, Mkoa una jumla ya ukubwa wa Kilometa za Mraba 41, 311 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.1.

***Jedwali Na. 1: Eneo kwa Halmashauri***


| Na. | Halmashauri | Eneo ($Km^2$) | Tarafa | Kata | Vijiji | Vitongoji | Mitaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bahi | 5,949 | 4 | 22 | 59 | 553 | 0 |
| 2 | Chamwino | 8,056 | 5 | 36 | 107 | 812 | 0 |
| 3 | Chemba | 7,653 | 4 | 26 | 114 | 491 | 0 |
| 4 | Dodoma Jiji | 2,576 | 4 | 41 | 0 | 0 | 222 |
| 5 | Kondoa | 4,640 | 2 | 21 | 84 | 380 | 0 |
| 6 | Kondoa Mji | 917 | 2 | 8 | 0 | 0 | 36 |
| 7 | Kongwa | 4,041 | 3 | 22 | 87 | 385 | 0 |
| 8 | Mpwapwa | 7,479 | 4 | 33 | 113 | 593 | 0 |
| | **Jumla** | **41,311** | **28** | **209** | **564** | **3,214** | **258** |

## 1.1 Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Dodoma una watu 3,085,625 ambapo Wanaume ni 1,512,766 na Wanawake ni 1,572,865. Idadi ya Watu kwa kila Wilaya imeoneshwa kwenye Jedwali Na.2.

*Jedwali Na. 2: Idadi ya Watu*

| Na. | Wilaya | Idadi ya Watu | Wanaume | Wanawake | Jumla ya Kaya |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bahi | 322,526 | 156,427 | 166,099 | 75,792 |
| 2 | Chamwino | 486,176 | 236,583 | 249,593 | 118,812 |
| 3 | Chemba | 339,333 | 170,837 | 168,496 | 75,050 |
| 4 | Dodoma | 765,179 | 373,440 | 391,739 | 214,331 |
| 5 | Kondoa | 325,297 | 164,532 | 160,765 | 73,073 |
| 6 | Kongwa | 443,867 | 214,475 | 229,392 | 101,761 |
| 7 | Mpwapwa | 403,247 | 196,466 | 206,781 | 99,004 |
| | **Jumla** | **3,085,625** | **1,512,760** | **1,572,865** | **757,823** |




*Kielelezo Na1: Mgawanyo wa Idadi ya Watu Ki-Wilaya kwa Mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022*

## 2.0 Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita Kisekta

Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Kwa Mkoa wa Dodoma, Mafanikio ya Serikali ya awamu ya Sita kwa kipindi cha miaka miwili (2021/22 – 2022/23) ni kama ifuatavyo:

## 2.1 Mpango na Bajeti ya Mkoa na Halmashauri

a) Bajeti ya Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri imeongezeka kutoka Shilingi **314,945,766,645** mwaka 2020/21 hadi Shilingi **372,065,282,000** mwaka 2022/23 sawa na **18%.** Aidha, ongezeko hili limesaidia kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi katika Mkoa wa Dodoma.

b) Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri imeongezeka kutoka Shilingi **61,503,000,000** mwaka 2020/21 hadi kufikia Shilingi **72,717,906,610 mwaka** 2022/2023 sawa na **18%.** Ongezeko hili limesaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza uwezo wa kujitegemea.

c) Fedha za miradi ya maendeleo kupitia mapato ya ndani kwa kigezo cha **40% & 60%** zimeongezeka kutoka shilingi **32,188,825,000** mwaka 2020/21 hadi kufikia shilingi **35,053,432,677** mwaka 2022/23 Sawa na **9%**. Ongezeko hili limesaidia kuboresha huduma za jamii kwa kujenga vituo vya afya 4 zahanati 12 na vyumba vya madarasa 135 kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.



*Picha Na. 1 Jengo la kitega Uchumi Mji wa Serikali Mtumba Halmashauri ya Jiji Dodoma kupitia Mapato ya Ndani*



*Picha Na. 2 Ujenzi wa kituo cha Afya Lenjulu Kongwa Kupitia Mapato ya Ndani*

d) Fedha za Mikopo ya Wanawake , Vijana na Watu Wenye Ulemavu (Asilimia 10) zimeongezeka kutoka Shilingi **4,682,593,000** mwaka 2020/21 hadi kufikia Shilingi **5,581,221,000** mwaka 2022/23 sawa na 19%. Ongezeko hili limesaidia kuongezeka kwa kiasi cha fedha kinachokopeshwa na idadi ya vikundi vinavyonufaika na mikopo inayotolewa na Halmashauri.



*Picha Na. 3 Mkuu wa Mkoa wa Dodoma akizindua zoezi la kukabidhi bodaboda na bajaji kwa vikundi Jiji la Dodoma*




*Picha Na. 4 Mkuu wa Mkoa akikabidhi mfano wa hundi kwa Vikundi vilivyonufaika na Mkopo Jiji la Dodoma*

e) Serikali Kuu imeidhinisha Bajeti ya shilingi **977,676,000** kwa mwaka 2022/2023 kwa ajili ya kuwalipa Waheshimiwa Madiwani posho za kila mwezi badala ya Fedha hizi kulipwa na Halmashuri. Aidha, Mpango huu wa Serikali Kuu kulipa Waheshimiwa Madiwani posho ***haujawahi kufanyika katika awamu zote zilizopita*** ambapo kwa sasa Waheshimiwa Madiwani wanapata posho za mwezi kwa wakati.

f) Halmashauri zimetenga Shilingi **250,800,000** kwa Watendaji wa Kata **209** ikiwa ni posho ya Madaraka kwa mwaka ambapo kila mwezi hulipwa shilingi **100,000** kwa kila Mtendaji**.** Aidha, Mpango huu wa kuwalipa Watendaji wa Kata ***haujawahi kufanyika katika awamu zote*** zilizopita ambapo kwa sasa wanapata posho zao kila mwezi kwa wakati.

g) Serikali Kuu imeidhinisha Bajeti ya Shilingi **36,000,000** kwa mwaka 2022/23 kwa ajili ya kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji posho za mawasiliano za kila mwezi. Aidha, Mpango huu wa Serikali Kuu kulipa Wenyeviti wa Vijiji ***haujawahi kufanyika katika awamu zote*** zilizopita ambapo kwa sasa Wenyeviti wa Vijiji wanapata posho za mawasiliano ya simu kila mwezi kwa wakati.

h) Ujenzi wa Nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa ambapo ujenzi

umegharimu jumla ya **Shilingi 784,719,950.** Ujenzi umekamilika kwa asilimia 100.



*Picha Na. 5 Ujenzi wa Nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa*

i) Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa na Mpwapwa ambapo ujenzi umegharimu jumla ya **Shilingi 600,000,000.** Ujenzi umefikia asilimia 95.



*Picha Na.6 Ujenzi wa Nyumba ya Katibu Tawala Wilaya ya Kondoa*



*Picha Na.7 Ujenzi wa Nyumba ya Katibu Tawala Wilaya ya Mpwapwa*

j) Ujenzi wa Ofisi 3 za Maafisa Tarafa za Zuzu, Kikombo na Hombolo Wilaya ya Dodoma ambao umegharimu jumla ya

Shilingi 450,000,000.00. Ujenzi umefikia asilimia 95.



*Picha Na. 8 Ujenzi wa ofisi ya Afisa Tarafa ya Kikombo Wilaya ya Dodoma*



*Picha Na. 9 Ujenzi wa ofisi ya Afisa Tarafa ya Zuzu Wilaya ya Dodoma.*

## 2.2 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)


### 2.2.1 Mafanikio

i. Makusanyo ya TRA yameongezeka kwa mwaka 2020/21-2022/23 kama ifutavyo;

***Jedwali Na. 3 Makusanyo ya TRA kwa kipindi cha 2020/21-2022/23***


| Mwaka | Makiso | Makusanyo | % |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 184,843,100,000 | 181,196,590,000 | 98 |
| 2021/22 | 200,189, 570,000 | 189,828,830,000 | 95 |
| 2022/23 | 109,816,650,000 | 113,247,090,000 | 103 |

ii. Kuongeza wigo wa walipa kodi kwa kufanikiwa kusajili walipakodi wapya 12,076 kwa kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Disemba 2022.




*Kielelezo Na. 2 : Usajili wa Walipa Kodi*

iii. Kuongeza usajili wa walipa kodi wapya 2237 wanaotumia mashine za kutolea stakabadhi za kielektroniki (EFD).




*Kielelezo Na. 3: Mashine za Risiti za Kielektroniki (EFD)*

iv. Kutoa elimu kwa walipa kodi 4, 499 ndani ya Mkoa wa Dodoma kuanzia Januari 2021 hadi Desemba, 2022 kama inavyosisitizwa na Serikali ya awamu ya sita ili kodi ilipwe bila shuruti.

*Picha Na. 10 TRA ikitoa Elimu kwa Mlipa kodi kwa wateja Wake.*

## 2.3 Sekta ya Elimu

### 2.3.1 Elimu ya Msingi

i. Idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa Darasa la Awali imeongezeka kutoka wanafunzi 71,590 mwaka 2020/21 hadi 72,927 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 1.87.

ii. Idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa Darasa la kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 78,858 mwaka 2020/21 hadi 90,301 Mwaka 2022/23 sawa na asilimia 14.51. Ongezeko hili limetokana na utekelezaji wa sera ya elimu Msingi bila malipo.

iii. Ufaulu wa wanafunzi katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) umeongezeka kutoka asilimia 76.19 mwaka 2020/21 hadi 83.01 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 6.82.

iv. Bajeti ya Fedha za Mpango wa Elimu bila Malipo kwa Shule za Msingi imeongezeka kutoka Shilingi 4,466,566,533.72 Mwaka

2020/21 hadi Shilingi 6,903,484,140.63 Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 54.56.

v. Idadi ya shule za Msingi za Serikali imeongezeka kutoka Shule 736 Mwaka 2020/21 hadi Shule 784 Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 6.52.



***Picha Na. 11 Shule Mpya ya Msingi Lugala iliyopo Halmashauri ya Chamwino iliyojengwa kwa fedha za Mradi wa TCRP.***

vi. Kuanzishwa kwa shule mbili za Msingi zinazofundisha kwa kutumia Lugha ya Kiingereza (English Medium) katika Halmashauri za Bahi na Dodoma Jiji.



***Picha Na. 12 Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Lugha ya Kiingereza Msangalale iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma***

vii. Idadi ya Vyumba vya Madarasa kwa Shule za Msingi imeongezeka kutoka Madarasa 5,812 Mwaka 2020/21 hadi 6,205 Mwaka 2022/23. Ongezeko la Madarasa 393 limetokana na ujenzi wa vyumba vya Madarasa 175 kupitia fedha za mradi wa TCRP Shilingi 3,500,000,000, ukamilishaji wa Madarasa 12 kupitia Mradi wa LANES yaliyogharimu Shilingi 240,000,000 ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 59 kwa kiasi cha Shilingi 787,500,000 kutoka Serikali na madarasa yaliyobaki yamejengwa kupitia Mapato ya ndani ya Halmashauri.



*Picha Na. 13 Vyumba vipya vya madarasa ya Msingi Njida iliyopo Halmashauri ya Kongwa yaliyojengwa kwa fedha za TCRP.*



*Picha Na. 14 Vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Simai iliyopo Halmashauri ya Mpwapwa fedha za TCRP*

### 2.3.2 Elimu ya Sekondari

i. Idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 29,788 Mwaka 2020/21 hadi 33,883 Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 13.58.

ii. Bajeti ya Fedha za Mpango wa Elimu bila malipo kwa Shule za Sekondari imeongezeka kutoka Shilingi 4,585,462,268.12 Mwaka 2020/21 hadi Shilingi 7,549,386,970.44 Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 64.63.

iii. Shule za Sekondari za Serikali zimeongezeka kutoka Shule 193 Mwaka 2020/21 hadi 218 Mwaka 2022/23. Hii ni sawa na ongezeko la Shule 25 kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 12.95.



***Picha Na. 15 Shule Mpya ya Sekondari Tura- Halmashauri ya Mji Kondoa iliyojengwa kwa Fedha za Mradi wa SEQUIP***

iv. Vyumba vya madarasa kwa Shule za Sekondari vimeongezeka kutoka Madarasa 2,226 Mwaka 2020/21 hadi 3,256 Mwaka 2022/23. Ongezeko la Madarasa 1,030 limetokana na ujenzi wa Madarasa 601 kwa kiasi cha shilingi 12,020,000,000 za mradi wa TCRP, madarasa 88 kupitia fedha za SEQUIP kiasi cha Shilingi 1,760,000,000, ukamilishaji wa Maboma 23 kwa kiasi cha Shilingi 287,500,000 kupitia fedha za tozo, ukamilishaji wa madarasa 18 kupitia fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha Shilingi 225,000,000 na madarasa yaliyobaki kupitia Mapato ya Ndani ya Halmashauri.



*Picha Na. 16 Vyumba vipya vya Madarasa katika Shule ya Sekondari Bumbuta -Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa yaliyojengwa kwa Fedha za Tozo*

v. Idadi ya walimu wanaofundisha Masomo ya Sayansi kwa Shule za Sekondari imeongezeka kutoka walimu 1,102 waliokuwepo Mwaka 2020/21 hadi kufikia walimu 1,295 Mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 17.51.

### 2.3.3 Chuo Kikuu cha Dodoma

#### 2.3.3.1 Mafanikio

a. Usajili wa Wanafunzi wa Shahada za awali katika Chuo umeendelea kukua kutoka wanafunzi 1,200 mwaka 2007 hadi 30,891 katika mwaka wa masomo 2021/22 wakiwemo wanafunzi kutoka nje ya nchi.

b. Miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa na Chuo inafikia Shilingi **bilioni 2.9**.

c. Katika mwaka wa masomo 2021/22, Serikali ilitoa mikopo kwa jumla ya Wanafunzi 25,670 yenye thamani yaShilingi **73, 242, 913,875** kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

d. Katika kipindi cha mwaka wa masomo 2022/23 mpaka kufikia Januari 2023, jumla ya wanafunzi 27,994 wameshapata mikopo yenye thamani ya Shilingi **76, 070, 892, 620**.

e. Katika kipindi cha 2020/21-2022/23, Chuo kimeendelea kutoa huduma za jamii katika Halmashauri za mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Mwanza, Iringa, Manyara na Shinyanga kwa kushirikiana na Idara za Afya za Halmashauri husika ambapo Jumla ya wananchi 66,089 walipata huduma hizo.

f. Katika kutekeleza kampeni ya kukijanisha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dodoma kimepanda miti 20,000, ikiwepo miti ya matunda, miti ya mapambo na kivuli.



*Picha Na.17: Upandaji wa Miti katika Chuo Kikuu cha Dodoma*

## 2.3.4 Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini

### 2.3.4.1 Taaluma

a) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa na kusajiliwa kila mwaka. Mwaka wa masomo 2022/23 kimesajili jumla ya wanafunzi **14,416** (wanaume **6,587** na wanawake **7,829**) ikilinganishwa na wanafunzi 10,652 ( wanaume 4,905 na wanawake 5,747) mwaka 2021/22;

b) Wahitimu wameendelea kuongezeka kila mwaka. Mathalani katika Mahafali ya **36** ya Chuo yaliyofanyika tarehe 2/16/ Desemba 2022 jumla ya wanafunzi **8,200** (wanaume **3,383** na wanawake **4,817)** walihitimu. Idadi

hii ya wahitimu ni sawa na ongezeko la asilimia **22.7** ikilinganishwa na wahitimu **6,684** (Wanaume **2,793** na Wanawake **3,891**) kwa mwaka 2020/21; na

c) Chuo kiliwezesha wahadhiri wake kuandika mada zilizomo kwenye vitabu viwili. Kitabu cha Kwanza kiitwacho ***"The Game Changer: President Magufuli's First Term in Office"*** ambacho kilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Januari, 2021 na kitabu cha pili kinaitwa ***"Continuity with Vision: The Roadmap to Success for President Samia Suluhu Hassan"*** kilichozinduliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (MB) tarehe 10 Novemba 2022 kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasimu Majaliwa Majaliwa (MB).

### 2.3.4.2 Utawala

a) Kuongezeka kwa idadi ya watumishi kutoka watumishi 348 (wanaume 227 na wanawake 121) mwaka 2020/21 hadi watumishi 368 (wanaume 241  wanawake 127 )mwaka 2022/23;

b) Kuendelea kupata hati safi katika Hesabu za Chuo zinazokaguliwa za kila mwaka;

c) Kupata tuzo ya Utendaji Bora katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala Bora nafasi ya Tatu. Tuzo hiyo ilitolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mwezi Mei, 2022 hapo Dodoma. Hii ni kutokana na Chuo kuwa na uzingatiaji mzuri wa kanuni, taratibu na sheria za kazi katika shughuli za usimamizi wa rasilimali watu huku;

d) Kupata tuzo ya Mshindi wa Tatu katika Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kutokana na mchango wa Kituo cha Ubunifu na Ujasiriamali kwa Jamii kama moja ya taasisi za elimu ya juu hapa nchini inayotoa mchango mkubwa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu cha Chuo kilichoanzishwa mwaka 2018. Tuzo hii ilitolewa katika Kongamano la sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilifanyika Jijini Dodoma mwezi Septemba, 2022;

e) Kuendelea kuwaendeleza watumishi kwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali sanjari na kuwajengea uwezo watumishi katika mfunzo ya muda mfupi;

f) Kuwawezesha watumishi kupitia Kitengo cha Masuala Mtambuka, kupata semina za mara kwa mara katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya maeneo hayo ni magonjwa yanayoambukiza, magonjwa yasiyo ambukiza, Utawala Bora na Uwajibikaji, mapambano dhidi ya rushwa na maandalizi ya kustaafu;

g) Kuongeza wigo kwa wadau wanaopata huduma za mafunzo ya muda mfupi na ushauri elekezi; na

h) Kuongeza kwa vya vifaa vya TEHAMA na matumizi ya mtandao kumesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za taasisi na kuongeza ufanisi katika kuendesha shughuli za Chuo na utoaji wa huduma kwa wateja.

**2.3.4.3 Maendeleo ya Miundombinu**

Uendelezaji wa miundombinu ya Chuo umezingatia miradi iliyopangwa na kuidhinishwa katika Mpango Mkakati wa Chuo wa mwaka 2021/22-2025/26. Jumla ya **Shilingi 9,000,000,000.00** zimetumika kugharamia utekelezaji wa miradi hiyo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,000,000,000.00** ni ruzuku kutoka Serikali kuu na **Shilingi 4,000,000,000.00** ni mapato ya ndani ya Chuo.

#### 2.3.4.4 Miradi iliyotekelezwa kwa kutumia Fedha za Ruzuku

Chuo katika mwaka wa fedha 2021/22 kiliidhinishiwa kutumia Shilingi **5,000,000,000.00** kutekeleza miradi 5 ya maendeleo kwa kutumia Fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo. Miradi hiyo ni: -

a) **Ujenzi wa Kumbi tatu za Mihadhara**

Kila Jengo lina ukumbi mmoja wa mihadhara wenye uwezo wa kukaa watumiaji 400 kwa wakati mmoja, vyumba vya madarasa viwili yenye uwezo wa kukaa watumiaji 200 kila moja na, vyumba vya ofisi vinane vyenye uwezo wa kuchukua watumishi watatu kila moja na vyoo 10. Kukamilika kwa mradi huu kumewezesha jumla ya wanafunzi 2,400 na watumishi 72 kutumia majengo haya kwa wakati mmoja.

Jumla ya gharama zote za miradi hii ni Shilingi **5,942,515,907.85.** Ujenzi wa miradi hiyo umekamilika.

b) **Ujenzi wa Mabweni mawili ya Wanafunzi wa Kike**

Kila bweni lina vyumba 52 vyenye uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi 204 kwa wakati mmoja, chumba cha kupumzikia (Common room) kimoja kikiwa na uwezo wa kuchukua watumiaji 30 kwa wakati mmoja na nyumba ya Msimamizi wa Bweni yenye vyumba viwili vya

kulala na eneo la kupumzikia (Sitting room), ofisi na stoo ya magodoro. Jumla ya gharama za mradi huu ni **Shilingi 3,810,132,465.84.**

### 2.3.4.5 Miradi iliyotekelezwa kwa kutumia Mapato ya Ndani ya Chuo

Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Chuo kwa kutumia mapato yake ya ndani kinatekeleza miradi mitano (5) ya maendeleo. Miradi hiyo ni: -

a) **Ujenzi wa Mgahawa**

Ujenzi wa mradi huu ulitekelezwa kwa kutumia mfumo wa Nguvu kazi (Force Account). Mgahawa huu umeanza kutumika na unauwezo wa kuchukua watu 200 kwa wakati mmoja. Gharama za mradi huu ni **Shilingi 435,239,691.45.**

b) **Ujenzi wa Jengo la Utawala**

Jengo hilo la Utawala lina ofisi 14 zenye uwezo wa kuchukua wafanyakazi 30 kwa wakati mmoja na chumba cha mikutano kimoja chenye uwezo wa kuchukua watumiaji 8 kwa wakati mmoja. Kama ilivyokuwa kwa mradi wa mgahawa, Mradi huu pia umetekelezwa kwa kutumia mfumo wa Nguvu Kazi (Force Account). Gharama za ujenzi wa mradi huo ni **Shilingi 397,482,925.43.**

c) **Ujenzi wa Jengo la Maktaba**
Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua ya utekelezaji. Mradi huu katika mwaka wa fedha 2021/22 ulitengewa S**hilingi 400,000,000.00** ili kuanza ujenzi wake.

d) **Kufidia Ardhi kwa Ajili ya Upanuzi wa Chuo - Mwanza**
Chuo kilitumia jumla ya **shilingi 1,728,039,000.00** kufidia ardhi yenye ukubwa wa ekari **59.07** na mali mbalimbali zikiwemo nyumba na miti katika eneo la Kitumba Wilaya ya Magu Mkoa wa Mwanza na kufanya eneo la Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa kuongezeka kutoka ekari 20 hadi ekari 79.07 zote zikiwa katika eneo moja.

e) **Kufidia Ardhi - Dodoma**
Chuo kimetoa fidia jumla ya **Shilingi 1,080,411,600.00** kupata ardhi yenye ukubwa wa **ekari 636.64** katika eneo la Nala.

### 2.3.4.6 Huduma Ushauri Uelekezi

Chuo kimetekeleza shughuli mbalimbali za ushauri, utafiti na uelekezi kwa lengo la kujenga uwezo wa taasisi na watu binafsi husika kwa lengo la kutatua changamoto za kimaendeleo za kijamii na kiuchumi.
Chuo kimetekekeleza shughuli 10 za Ushauri na Uelekezi katika maeneo yafuatayo; mipango mikakati, kuandaa mipango ya usimamizi ya

mazingira; na kuchunguza hali ya kijamii na uchumi kwa ngazi ya kaya kwenye jamii zinazoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

#### 2.3.4.7 Miradi

Chuo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) tumetekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kiuchumi wananchi. Baadhi ya miradi hiyo ni Pamoja na: -

a) Uandishi wa taarifa ya Maendeleo ya Mwanadamu Tanzania (Tanzania Human Development Report 2022).

b) Uandishi wa Mwongozo wa Uwekezaji wa Tanzania "Tanzania National Investment Guide" kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Centre).

c) Tathmini ya mkakati wa kugharamia (Financing Strategy), utekelezaji wa mpango wa tatu wa Taifa kwa kushirikina na Wizara ya Fedha na Mipango. Uandishi wa taarifa umekamilika.

d) Uandaaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa 2021/2022 hadi 2025/2026 uliozinduliwa tarehe 29/06/2021.

e) Kukusanya takwimu kwa ajili ya upembuzi yakinifu (feasibility study) wa Miradi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

f) Kuandaa taarifa ya Tathmini ya ushirikishwaji wa Watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati (Assessment of Tanzania Local Content) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

#### 2.3.4.8 Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET)

Chuo kinatekeleza mradi wa HEET kwa lengo la kuboresha Mazingira ya kufundishia, kujifunzia kwa kujenga jengo moja la Taaluma katika eneo la Miyuji Kampasi Kuu ya Dodoma, Kuboresha mitaala, kuwajengea wahadhiri uwezo kwa kuwapeleka kufanya mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya uzamivu na kuboresha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunzia. Chuo kimetengewa jumla ya Shilingi **6,853,521,008.77.**

### 2.3.5 Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi (VETA)

i. VETA imepokea Shilingi **1,334,039,238.60** kwa ajili ya ujenzi vya you vya Elimu ya Ufundi Stadi vya Wilaya ya Bahi na Chemba kupitia fedha za mradi wa TCRP na ESCJ. Kupitia fedha hizi vyuo hivi vipo katika hatua ya umaliziaji ili vianze kudahili wanafunzi.



***Picha Na. 18: Muonekano wa bweni la wasichana katika chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Bahi***

ii. VETA imeendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara na wajasiliamali wadogo wadogo katika mkoa wa Dodoma ambapo katika awamu hii ya sita tumefanikiwa kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara ndogo ndogo za vyakula na vinywaji wapatao arobaini (40) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Kondoa.

iii. VETA ilipokea Shilingi 700,196,000 toka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya utengenezaji wa samani za vyuo vya ufundi stadi vya Wilaya za Bahi na Chemba.

## 2.4 Sekta ya Afya

Hali ya upatikanaji wa huduma bora za afya katika Mkoa wa Dodoma imeendelea kuimarika na kupata mafanikio kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji

katika maeneo ya utoaji huduma na ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya kama ifuatavyo:

a. Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeongezeka kutoka vituo 429 mwaka 2020/21 hadi 467 mwaka 2022/23. Ongezeko hili limesaidia Wananchi kuwa na uhakika wa kupata matibabu.

    i. Idadi ya zahanati imeongezeka kutoka **375** hadi **404** sawa na **7%.**



*Picha Na.19 Zahanati ya Manchali B-Chamwino*



*Picha Na. 20 Zahanati ya Tubugwe Kongwa*

    ii. Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka **43** hadi **47** sawa na **8.5%.**



*Picha Na. 21 Ujenzi wa Kituo cha Afya Farkwa- Chemba DC*



*Picha Na. 22 Ujenzi wa Kituo cha Afya Farkwa- Chemba DC*

iii. Hospitali za Halmashauri za Wilaya zimeongeka kutoka 11 hadi **16** sawa na **31%.**



**Picha Na. 23** *Majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Chemba*

b. Vituo vya kutolea huduma za dharula za upasuaji vimeongezeka kutoka vituo 29 mwaka 2020/21 hadi 36 mwaka 2022/23. Uwepo wa vituo hivi umeboresha huduma za uzazi katika jamii ili kuhakikisha wajawazito wote wanajifungulia katika vituo vya huduma bila kusafiri umbali mrefu.



***Picha Na. 24 Vifaa vya huduma za watoto wachanga na upasuaji Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.***

c. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na Vifaa tiba zimeongezeka kutoka Shilingi 4,771,595,155.00 kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia shilingi 5,280,524,774.00 mwaka 2022/23. Fedha hizi zimesaidia vituo kupata dawa kwa gharama nafuu.

d. Kuimarika kwa uchunguzi wa magonjwa ya milipuko ukiwamo ugonjwa wa UVIKO-19 ambapo upimaji wa UVIKO- 19 unafanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, jumla ya wagonjwa/wateja 5,989 wamefanyiwa uchunguzi wa ugonjwa huo.

e. Kufikia lengo la utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 ambapo jumla ya wananchi 1,663,827 walichanjwa kati ya walengwa l, 385,385 (113%). Mkoa wa Dodoma ulikuwa wa kwanza kufikia lengo la kitaifa.

f. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 88 mwaka 2020/21 hadi 51 mwaka 2022/23.Upungufu huu umetokana na utoaji wa elimu ya huduma za uzazi kwa watumishi wa afya, kuimarisha mfumo wa Rufaa na kuongozeka kwa vituo vya huduma za Afya vinavyotoa huduma za uzazi na upasuaji.

g. Kuanza kufanya kazi kwa kituo cha Damu Salama Kanda ya Kati kilichopo Mkoani Dodoma, uwepo wa kituo hiki umerahisisha upatikanaji wa damu salama na mazao ya damu, na hivyo kusaidia katika kupunguza vifo vitakanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama ambazo zilikuwa zinatumika kusafirisha sampuli za damu kwenda Maabara Kuu ya Taifa iliyopo Dar Es Salaam. Kituo hiki kimegharimu jumla ya Shilingi 2,678,848,589.60, gharama hizi zinajumuisha ujenzi na vifaa tiba.




*Picha Na. 25: Kituo cha Damu Salama kanda ya Kati-Dodoma*

h. Mkoa umepata Makao ya Taifa ya kuhudumia watoto walio katika mazingira hatarishi yaliyopo Kikombo. Kwa sasa kuna watoto 51 ambapo kituo kina uwezo wa kutunza watoto 250



*Picha Na. 27 Makao ya Taifa ya kulelea watoto Kikombo*

i. Kuongezeka kwa idadi ya nyumba za watumishi kutoka nyumba 421 mwaka 2020/21 hadi 445 mwaka 2022/23.




*Picha Na. 28 Nyumba ya Mtumishi kituo cha Afya Chifutuka Wilaya ya Bahi*



*Picha Na. 29 Nyumba ya Mtumishi Hospitali ya Wilaya Chemba*

j. Kusimikwa kwa mashine sita za mionzi (X-ray mashine) hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma katika Halmashauri 5 (Bahi, Chamwino, Chemba, Dodoma na Kondoa)





*Picha Na. 30: X-Ray Machine kituo cha Afya Hombolo Dodoma Jiji*

k. Serikali imetoa fedha shilingi 900,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya matatu ya kutoa huduma za dharula (EMD) katika Hospitali za Halmashauri za Bahi, Kondoa Mji na Kongwa.







*Picha Na. 31 Jengo la EMD-Halmashauri ya Wilaya ya Bahi*

l. Serikali imetoa fedha Shilingi 810,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya mawili ya kutoa huduma kwa wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shillingi 560,000,000

na Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa Shilingi 250,000,000.



*Picha Na. 32 Jengo la huduma za wagonjwa mahututi Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa*

m. Ajira za watumishi wa kada mbalimbali za afya zimeongezeka kutoka watumishi 1,878 mwaka 2020/21 hadi 2,698 mwaka 2022/23.

n. Kuongezeka kwa huduma za uchunguzi katika Mkoa ambapo huduma za CT-Scan zinatolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Jengo la huduma ya mionzi pamoja na usimikaji wa CT-Scan vimegharimu Shilingi 300,000,000.00



*Picha Na. 33 Machine ya CT-Scan katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa*

o. Kusimikwa kwa mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni katika Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Mitambo hiyo itaongeza upatikanaji wa hewa tiba ya Oksijeni na kuwasaidia wananchi wa Dodoma.

### 2.4.1 Hospiatli ya Rufaa ya Mkoa

**a. Ongezeko la Vifaa tiba, dawa na vitendanishi**

Hospitali imefanikiwa kuhakikisha uwepo wa dawa za msingi na vifaa tiba vya kisasa ambavyo havikuwepo hapo awali kama mashine ya CT-scan, vifaa vya wagonjwa wenye dharula na mahitaji maalum.



***Picha Na. 34: Baadhi ya vifaa vya kisasa kwa ajili ya jengo la Dharula shilingi 691,000,000***



*Picha Na. 35: Vifaa kwa ajili ya uchunguzi (maabara) na vifaa vya huduma za dharura*



*Picha Na. 36: Baadhi ya vifaa kwa ajili ya matibabu ya kibingwa na upasuaji*

## b. Kusimikwa vifaa vya CT -Scan kwa gharama za Shilingi 1,800,000,000



*Picha Na.37: CT- Scan*

## c. Jengo la wagonjwa wenye uhitaji wa uangalizi maalum (ICU)

Jengo jipya la kutolea huduma kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU) kwa gharama za shilingi 725,000,000



*Picha Na. 38: Jengo la Uangalizi Maalum*



***Picha. 39: Muonekano wa ndani wa jengo la kuhudumia wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu.***

d. Jengo la wagonjwa wa nje na dharula (EMD) usimikaji wa mtambo wa kutengeneza hewa tiba (Oksijeni) kwa wagonjwa wenye uhitaji maalum (EMD) kwa gharama ya Shilingi 100, 000, 000.




***Picha Na. 40: Muonekano wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa Dharula (EMD) lililoboreshwa***

## 2.4.2 Hospitali ya Benjamin Mkapa

Hospitali ya Benjamin Mkapa imepiga hatua kubwa ndani ya kipindi cha awamu ya sita kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka Bajeti na usimimizi, na haya ni maeneo ya mafanikio:-

## 2.4.3 Huduma zinazotolewa na Hospitali

### a. Upandikizaji Figo

Hospitali imefanikiwa kupandikiza wagonjwa wa figo 31

**b. Moyo**

i. Jumla ya wagonjwa waliohudumiwa CathLab 758
ii. Upandikizaji Betri 12
iii. Watoto waliozibwa matundu kwenye Moyo 10
iv. Stent 52

**c. Vipandikizi Kwenye Magoti & Nyonga (Hip and total Knee Replacement)**

Wamenufaika wananchi 53

**d. Ubongo Na Mishipa Ya Fahamu**

i. Upasuaji wa jumla 964
ii. Upasuaji wa Ubongo 549
iii. Upasuaji uti wa mgongo 415

### 2.4.4 Mapato

#### 2.4.4.1 Mapato kutoka Serikali Kuu - 30,488,380,926.81

a. Mishahara Shilingi 17,825,011,249.77
b. Matumizi mengineyo Shilingi 2,380,193,539.26
c. Posho Watarajali Shilingi 1,192,276,000.00
d. Nyumba za watumishi na Mionzi Tiba Shilingi 6,9068,960,137.78
e. Mradi wa TCRP shilingi 2,181,940,000.00

#### 2.4.4.2 Mapato ya ndani Shilingi 43,366,164,099.75

***Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani***

| NA | Miundombinu/Mradi/Huduma | Gharama |
|---|---|---|
| 1 | Mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni | Billioni 1.1 |
| 2 | Nyumba 40 za watumishi(nyumba hizi zipo katika mradi wa NHC Iyumbu) | Billioni 3.11 |
| 3 | Uanzishwaji wa huduma ya upandikizaji Uloto | Billioni 1 |
| 4 | Ununuzi wa Gari la Watumishi | Millioni 220 |

Hospitali ya Benjamin Mkapa ilipokea Bilioni 2.07 kutoka kwenye fedha za Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 na zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

***Jedwali Na. 5. Mchanganuo wa Matumizi ya fedha TCRP***

| Na | Mradi/Shughuli | Gharama | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukarabati wa chumba cha ICU | 166,280,147.22 | Ukarabati umekamilika |
| 2 | Kununua vifaa vya ICU&EMD | 1,000,000,000 | Manunuzi yamefanyika |
| 3 | Unuzi wa gari la wagonjwa la kisasa | 250,000,000 | Ununuzi wa gari unafanywa na Wizara |
| 4 | Unuzi wa gari la wagonjwa la kawaida | 180,000,000 | Ununuzi wa gari unafanywa na Wizara |
| 5 | Ununuzi wa Digital X-Ray | 304,000,000 | Manunuzi yamefanyika |
| 6 | Ukarabati wa | 116,000,000 | Ukarabati |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | chumba cha Digital X-Ray | | umekamilika |
| 7 | Ununuzi wa Apheresiss Mashine | 150,000,000 | Mashine imenunuliwa |
| 8 | Ununuzi wa Mashine ya Extraction ya Maabara | 150,000,000 | Mashine imenunuliwa |
| 9 | Kuanzisha huduma ya Telemedicine | 151,326,023 | Huduma imeanzishwa |
| 10 | Kuwezesha mafunzo ya Critical Care, Emergency and imaging | 36,000,000 | Mafunzo yameshafanyika |
| **Jumla** | | **2,073,606,170.22** | |

**Miradi inayoendelea na Ujenzi**

**Ujenzi wa Jengo la Mionzi Tiba**

Mradi utagharimu Shilingi Bilioni 28. Serikali imelipa Shilingi Bilioni 2.9 kwa mkandarasi.



*Picha Na. 41: Jengo la Mionzi Tiba*

### 2.4.5 Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ilipokea jumla ya Shilingi bilioni **5.551** ikiwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi zilitolewa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zikilenga jitihada za Serikali za kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Fedha zililenga kukamilisha ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa miundo mbinu chakavu ya Hospitali, manunuzi ya vifaa na vifaa tiba pamoja na mafunzo kwa wataalam na watumishi wa Hospitali, kama inavyoainishwa hapa chini.

*Jedwali Na.6: linaonesha fedha zilizotengwa kwa mwaka 2022/23;*

| S/N | Maelezo ya Mradi | Fedha Zilizotengwa |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Majengo a ICU na EMD | 750,000,000 |
| 2 | Manunuzi ya Vifaa Tiba vya Majengo ya ICU Na EMD | 1,580,630,000 |
| 3 | Ukarabati na Ujenzi wa Majengo | 3,200,000,000 |
| 4 | Mafunzo ya Wataalamu | 20,370,000 |
| 5 | Ushauri Elekezi | 300,000,000 |
| | **Jumla** | **5,551,000,000** |

Fedha hizi zilipokelewa kwa awamu tofauti, kuanzia mwezi Februari 2022 hadi Mei, 2022 na zimetumika kwa mtindo wa kazi kwa kufuata Mwongozo wa PPRA wa ketekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati kwa njia ya "Force Account"

**a. Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu**

Hospitali kupitia fedha iliyotolewa na Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe.Dkt. Samia Suluhu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali, ambapo, miradi mbali mbali ya ujenzi mpya pamoja na ukarabati wa miundo mbinu chakavu imekuwa ikiboreshwa.



*Picha Na. 42: Jengo la EMD kwa taswira tofauti*



*Picha Na. 43: Jengo la wagonjwa Mahututi (ICU)*



*Picha Na: 44: Vyumba 20 vya kliniki ya kutolea huduma kwa wateja*



*Picha Na. 45: Ukarabati wa majengo wodi za Isanga himaya ya wanaume*

## 2.5 Sekta ya Maji

### 2.5.1 DUWASA

a. Uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka wastani wa lita 61.5 Milioni Mwaka 2020/21 hadi lita 67.8 Milioni kwa siku Mwaka 2022/23. Ongezeko hili la uzalishaji limetokana na kukamilika kwa miradi mipya ya maji yenye thamani ya Shilingi bilioni 9.14.





***Picha Na. 46: Miradi Mipya ya Maji Jiji la Dodoma***

b. Wateja wa maji safi wameongezeka kutoka 54,124 Mwaka 2020/21 hadi 72,795 Mwaka 2022/23 sawa  na ongezeko la asilimia 34.49.

c. Upotevu wa Maji umepungua kutoka wastani wa 39.1% Mwaka 2020/21 hadi 28.3% 2022/23.

d. Makusanyo ya maduhuli yameongezeka kutoka wastani wa Shilingi. 1.6 Bilioni mwaka 2020/21 hadi Shilingi 2.3Bilioni Mwaka 2022/23.

e. Ukarabati wa Mtandao chakavu wa Maji Taka umefanyika katika eneo la Area C na D ili kuondoa adha ya harufu mbaya na kufurika Maji taka Mitaani mara kwa mara. Jumla ya

Kilometa 19 zimebadilishwa na chemba 1,005 zimejengwa kufikia Desemba, 2022.





*Picha Na. 47: Uboreshaji wa huduma ya Majitaka – Halmashauri ya Jiji la Dodoma*

f. Upatikana wa maji safi umeongezeka kutoka 42% mwaka 2020/21 hadi 87% Mwaka 2022/23 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, kutoka 44% hadi 88% kwa Kongwa na Bahi kutoka 37% hadi 95%.





*Picha Na. 48: Huduma ya Maji safi - DUWASA*

### 2.5.2 RUWASA

Upatikanaji wa huduma ya Maji vijijini kwa Mkoa wa Dodoma umefikia wakazi 1,393,167 sawa na asilimia 65.1 hadi kufikia Septemba 2022 ya kadirio la wakazi 2,141,601. Aidha, ofisi hii imepokea jumla ya kiasi cha Shilingi 21,569,406,201.60 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Taarifa ya mafanikio ya sekta ya maji katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita (06) ni haya yafuatayo:

i. Uendelezaji wa vyanzo vya maji (uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa) kwa kutumia vyanzo vikuu vilivyooneshwa katika jedwali hapo chini

***Jedwali Na. 8: Uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa kwa kutumia vyanzo vikuu***

| **Mwaka wa Fedha** | **PbR** | **Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF)** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 2,091,993,179.19 | 4,779,769,268.87 | 6,871,762,448.06 |
| 2021/2022 | 3,977,026,334.22 | 5,410,217,597.50 | 9,387,243,931.72 |
| 2022/2023 | | 5,310,399,821.82 | 5,310,399,821.82 |

ii. Uchimbaji wa visima (*boreholes*) virefu 34 katika Mkoa wa Dodoma







***Picha Na. 50: Kituo cha maji Mauno na Lambo la Mifugo Kikore Wilaya ya Kondoa***

iii. Ujenzi wa Mabwawa 2 ya maji katika Mkoa wa Dodoma

iv. Ujenzi wa miradi 10 ya maji inayotumia mtandao wa bomba




***Picha Na. 51; ujenzi wa tenki lita 280, 000 Bicha Kondoa Mji***



***Picha Na. 52.: Ujenzi wa tenki la maji Bukulu Kondoa.***

## 2.6 Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

### 2.6.1 TANROADS

Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dodoma inahudumia jumla ya Km **1,707.22.** Mchanganuo wa Mtandao huu wa Barabara ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 01

***Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa mtandao wa barabara mkoani.***

| **Na** | **Aina ya barabara** | **Lami** | **Changarawe** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Barabara kuu | 552.19 | 0 | 552.19 |
| 2 | Barabara za Mkoa | 37.18 | 1,117.85 | 1,155.03 |
| | **Jumla** | **589.37** | **1,097.38** | **1,707.22** |

Mkoa pia una jumla ya madaraja 332 kati ya hayo madaraja 155 yapo katika Barabara Kuu na 177 yapo katika Barabara za Mkoa.

Hadi mwisho wa Mwezi Disemba, 2022 hali ya mtandao wa barabara ilikuwa kama ifuatavyo:

**Barabara za lami**:

Asilimia **89.20%** ziko kwenye hali nzuri, asilimia **6.54%** ziko kwenye hali ya kuridhisha na asilimia **4.26%** ziko kwenye hali mbaya.

**Barabara za changarawe**:

Asilimia **79.87%** ziko kwenye hali nzuri, asilimia **12.67%** ziko kwenye hali ya kuridhisha na asilimia **7.46%** ziko kwenye hali mbaya

a. **Miradi ya Maendeleo iliyo katika Hatua za Usanifu**

**i.** Ujenzi wa barabara za mizunguko ya ndani *(Inner Ring Roads & Middle Ring Road) ndani ya Jiji la Dodoma* zenye urefu wa Km 63.2 kwa thamani ya **Shilingi bilioni 1.1.** Kazi ya Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko wa ndani (Inner Ring Roads) zenye urefu wa Km 16 imekamilika.

**ii.** Kuanza ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa kati ndani ya Jiji la Dodoma (Dodoma City Middle Ring Roads (km 47.2**)** yenye thamani ya milioni **684, 400,000**. Kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko wa kati (Middle Ring Roads) zenye urefu wa Km 23 umekamilika.

**iii.** Kukarabati barabara za kuunganisha na Reli ya SGR (Gulwe, Igandu, Ihumwa,Kizota, Zuzu na Bahi) wenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.6. Kazi ya usanifu wa kina wa barabara hizi umekamilika na zabuni ya kazi hizi zipo katika maandalizi ya kutangazwa.

iv. Ujenzi wa barabara ya Ihumwa – Hombolo (24km) kwa Kiwango cha Lami yenye thamani ya Shilingi milioni 200. Mhandisi Mshauri anaendelea kazi ya usanifu.

v. Ujenzi wa Daraja la Godegode (Dodoma) lenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5. Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi imekamilika na taratibu za kusaini mkataba zinaendelea.

**vi.** Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mpwapwa – Gulwe – Chipogoro (sehemu ya Kibakwe - Chipogolo) Km75.84. kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika kwa gharama ya Shilingi 710, 000, 000. Mhandisi mshauri anaendelea na usanifu na kazi ambapo atakamilisha ifikapo Machi, 2023.

**vii.** Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kelema Maziwani katika barabara ya Kondoa - Bicha – Dalai wenye thamani ya Shilingi 172, 700, 000.00. Mhandisi Mshauri amekamilisha usanifu wa kina na ameshawasilisha rasimu ya usanifu kwa ajili ya mapitio. Aidha Serikali imetenga Shilingi 600, 000, 000 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**viii.** Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ujenzi wa daraja la Munguri katika barabara ya Kondoa- Mtryangwi /Gisambalag wenye thamani ya Shilingi 480, 050, 000. Mhandisi Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu na anaendelea na usanifu wa kina. Aidha Serikali

imetenga **Shilingi 600, 000, 000** kwa ajili ya kuanza ujenzi.

ix. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ujenzi wa daraja la Mwanjiri na Suguta katika barabara ua Pandambili - Mlali - Ng'ambi, R.470 wenye thamani ya shilingi 190, 600, 000. Mhandisi Mshauri amekamilisha Usanifu wa kina na ameshawasilisha rasimu ya usanifu kwa ajili ya mapitio. Serikali imetenga jumla ya Shilingi 600, 000, 000 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

x. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ujenzi wa daraja la Nzali (Chilonwa) katika barabara ya Chamwino Ikulu Jct - Dabalo – Itiso kwa gharama ya Shilingi 177, 6000, 000. Mhandisi Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu na anaendelea na usanifu wa kina na kazi itakamilika Machi, 2023. Serikali imetenga Shilingi **600, 000, 000** kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**b. Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Mkoa**

**i.** Ujenzi wa Daraja la Baura (60m) wenye thamani ya shilingi bilioni 5.4. Ujenzi wa Daraja la Baura (60m) na barabara za maingilio (1.5km) katika barabara ya Gubali - Haubi umekamilika Aprili,

2022. Gharama za Mhandisi Mshauri ni Shilingi 706, 525, 000.

ii. Ujenzi wa barabara ya Mbande – Kongwa Junction – Mpwapwa, sehemu ya Kongwa – Mpwapwa (km 30).

Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha Lami wa Barabara ya Kongwa Jct- Mpwapwa (Mwanakianga – Ng’ambi km 5.0) kwa gharama ya Shilingi bilioni 8.8. Ujenzi unatekelezwa kwa awamu mbili awamu ya kwanza (Unconditional part 2km) kwa Gharama ya **Shilingi bilioni. 5.1**. Hadi kufikia Machi, 2022, Mkandarasi amekamilisha kazi za awamu ya kwanza kwa **asilimia 100** na amelipwa fedha zote. Aidha mkandarasi ameanza utekelezaji wa awamu ya pili (Conditional part 3km) ambao umepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2023.

iii. **Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kwa gharama ya Shilingi bilioni 3.6**. Mradi umekamilika.

**iv. Kukamilisha Ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye eneo la Ikulu ya Chamwino kwa gharama ya Shilingi bilioni 67.3. Ujenzi unafanyika kwa awamu.** Mkandarasi amekamilisha kazi zote za awamu ya kwanza na awamu ya pili Kwa sasa anaendelea na kazi za awamu ya tatu ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 10 na kazi zote zimepangwa

kukamilika mwanzoni mwa mwezi wa Septemba, 2023.

v. **Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Chamwino Ikulu hadi Msanga (1km) kwa gharama ya Shilingi 780, 000, 000.** Ujenzi umekamilika.



*Picha Na. 53: Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Chamwino Ikulu hadi Msanga*

### c. Miradi Midogo ya ukarabati wa Barabara Kwa Kiwango

Miradi ya barabara ya Changarawe imekarabatiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 13.8 katika Mkoa wa Dodoma. Hadi kufikia Agosti 2022 Miradi yote ya ukarabati wa barabara kutoka mfuko wa Barabara na Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imekamilika kwa asilimia 100.

d. **Miradi ya Usanifu Kitaifa**

i. **Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na uaandalizi ya Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mtera na Barabara za maingilio (KM 6)** wenye thamani ya shilingi bilioni 1.4. Mhandisi Mshauri amekamilisha usanifu wa kina na kazi ya maandalizi ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi imeanza.

ii. **Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa Kiwango cha lami barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430) kwa thamani ya Shilingi bilioni 2.5.** Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kwa ajili ya Ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika tangu Disemba, 2020. Mradi umetangazwa chini ya Mpango wa Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (EPC+F) na upo katika hatua za manunuzi.

iii. **Upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 263);**
Mhandisi mshauri anaendelea na usanifu. Aidha, amewasilisha rasimu ya awali ya uchumi na hali ya mafuriko katika Mji wa Kibaigwa na Dumila ili kupata maoni ya Wakala.

iv. **Upanuzi wa Barabara ya Kuu zinazoingia na kutoka Jiji la Dodoma**

**Usanifu wa barabara hizi unaendelea kama ifuatavyo: Dodoma – Iringa (km 50); Dodoma – Singida (km 50); na Dodoma – Babati (km 50) kwa gharama ya bilioni 2.0.** Utekelezaji wa barabara hizi umepangwa kutekelezwa kwenye mpango wa ujenzi wa Barabara za Dodoma chini ya ufadhili wa benki ya Dunia. Usanifu wa kina unaendelea kutekelezwa.

**e. Miradi ya Ujenzi Kitaifa**

i. Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (Outer ring road) yenye urefu wa Km 112.3 unatekelezwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:

**(a) LOT 1: Nala- Veyula- Mtumba- Ihumwa bandari kavu (KM 52.3)** kwa gharama ya Shilingi 100, 840, 778, 592. Mradi umefika asilimia 14.7 na mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2024. Aidha, Serikali imelipa fidia kwa wananchi **1,081** kwa jumla ya Shilingi **9, 470, 848, 259** ili kupisha ujenzi wa mradi huu.

**Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa nje sehemu ya Veyula- Nala**




*Picha Na. 54: Ujenzi wa barabara ya mzunguko wan je sehemu ya Veyula- Nala.*

**(b) Mradi Lot 2: Ihumwa Bandari Kavu – Matumbulu – Nala (60.0km)** kwa gharama ya Shilingi 120, 860, 638, 209.50. Mradi umeanza kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika ifikapo Machi, 2025. Aidha, Serikali imeshalipa fidia kwa wananchi **1,158** kwa jumla ya Shilingi **6,876,266,859.00** ili kupisha ujenzi.

## Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa nje sehemu ya Matumbulu- Nala




*Picha Na. 55: Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje sehemu ya Matumbnulu- Nala*

ii. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa – Msalato Dodoma kwa gharama ya Shilingi 165, 627, 031, 495.

Kiwanja kipo umbali wa kilomita 10 kaskazini mashariki mwa Jiji la Dodoma. Kiwanja kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa miundombinu ambayo itajumuisha sehemu ya kurukia ndege (Runway), sehemu ya kupaki ndege (Apron) na Njia ya ndege (Taxiway). Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa majengo ambayo itajumuisha miundombinu yote ya Majengo. Mkandarasi kwa ajili ya awamu ya kwanza anaendelea na kazi na amefikia asilimia 14.5 na mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili, 2025.

Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi awamu ya pili amepatikana na yupo kwenye maandalizi ya ujenzi. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo 2025. Aidha, Serikali imeshalipa fidia kwa wananchi **1,924** kwa jumla ya **Shilingi bilioni 15.2** ili kupisha ujenzi wa mradi huu. Vilevile, Wananchi **10** wamefanyiwa uhakiki na wanasubiri malipo yao ya fidia. Serikali pia imetenga jumla ya Shilingi **bilioni 2.4,4** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

iii. Barabara ya Ntyuka Jct. - Mvumi - Kikombo Jct (Km 76) na Chololo - Mapinduzi (Makao makuu ya Jeshi) (5 Km) kwa gharama ya shilingi 841, 100, 000.

Kazi ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Ntyuka Jct. - Mvumi - Kikombo Jct (Km 76) na Chololo - Mapinduzi (Makao makuu ya Jeshi) (5 Km) umekamilika.

Barabara hii itajengwa kwa awamu, katika awamu ya kwanza jumla ya **Km 25** zitajengwa ambazo ni sehemu ya barabara kutoka Dodoma **(Ntyuka Jct) – Mvumi Makulu (km 8.6)** na sehemu ya barabara kutoka Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (Makao makuu ya Jeshi) (km 16.4) kwa gharama ya Shilingi bilioni 38.2. Ujenzi unatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba, 2024.

Mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa ujenzi na amefika asilimia **10.5** ya utekelezaji. Aidha, Serikali imetenga jumla ya Shilingi **bilioni 4.6** kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huu.

### 2.6.2 TARURA

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa **km 7540.94** ambapo **km2702.11** ni barabara za Makusanyo (Collector roads), **km 3938.27** ni barabara za Mlisho (Feeder roads) na **km 900.56** ni barabara za Jamii (Community roads).

Sehemu kubwa ya mtandao huu ni ya tabaka la udongo na changarawe ambapo sehemu hii ina jumla ya urefu wa **Km 7314.315** sawa na asilimia **96.99** ya mtandao wote wa barabara. Aidha, barabara zilizopo katika tabaka la lami na zege ni **km 226.625** sawa na asilimia **3.0** tu ya mtandao wote wa barabara.

i. Matengenezo ya mtandao wa barabara umeongezeka katika kipindi cha mwaka 2021/22 ukilinganisha na mwaka 2020/21 katika mchanganuo ufuatao:

***Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa barabara na madaraja***

| **Mwaka wa Fedha** | **Kiwango cha lami (km)** | **Kiwango cha Changarawe (km)** | **Madaraja (Na)** |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 1.5 | 260.57 | 2 |
| 2021/2022 | 33 | 698.88 | 5 |
| 2022/2023 | 31.36 | 579.76 | 6 |



*Picha Na 56: Ujenzi wa barabara ya Nzuguni-Mahomanyika 1.55km katika Jiji la Dodoma*



*Picha Na. 57: Ujenzi wa barabara ya Ali Hassani Mwinyi yenye urefu wa km 1.2 Wilaya ya Chamwino*

ii. Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya barabara imeongezeka kutoka shilingi bilioni 20.40 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 55.60 mwaka 2022/23.

iii. Mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa. **km 7540.94**. unatengenezwa na kupitika katika kipindi chote cha mwaka.

## 2.6.3 LATRA

Kufuatia uwekezaji wa serikali katika miundombinu mbalimbali ya barabara mkoani Dodoma, Mamlaka ya Mawasiliano Nchi Kavu (LATRA) kwa kushirikiana na taasisi ambao ni wadau wa usafiri na usafirishaji imeweza kufungua njia mbalimbali za usafiri mkoani na zile zinazoiunganisha Dodoma kutoka mikoa mingine.

### 2.6.3.1 Usafiri wa ndani ya Mkoa

1) Ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mji wa Dodoma mamlaka imeendelea kuanzisha njia mbalimbali za usafiri wa daladala ndani ya mkoa ili kusogeza huduma ya usafiri kwa wananchi katika maeneo mapya kulingana na kasi ya ujenzi wa miundombinu unaoendelea.
2) Katika kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari Mamlaka imeacha kusajili magari mapya aina ya hiace hivyo kuweka mkazo katika

kusajili magari yenye uwezo wa kubeba abiria kuanzia 25 na kuendelea.

3) Mamlaka pia imeendelea kutoa leseni za usafirishaji kwa pikipiki, bajaj, taxi za kawaida na taxi mtandao ambazo zinatoa huduma kwa njia ya kukodiwa.
4) Leseni za pikipiki na Bajaj zinatolewa na Halmashauri za majiji, miji na wilaya kwa mujibu wa Randama ya Makubaliano iliyosainiwa kati ya Halmashauri za Wilaya na LATRA.

#### 2.6.3.2 Usafiri wa Magari ya masafa marefu.

1) Katika kuhakikisha huduma ya usafiri ni bora na yenye kukidhi matakwa ya huduma, LATRA mkoa wa Dodoma imeweza kufungua njia za mabasi ya masafa marefu kwa kuwezesha kuwa na huduma ya usafiri wa Basi kwenda mikoa yote ya Tanzania Bara.
2) Katika kusimamia usalama wa huduma Mamlaka imeendelea kusisitiza kutotoa leseni kwa msafirishaji ambae gari lake halijafungwa kifaa cha kufuatilia mwenendo wa gari (VTD).
3) Katika kuendelea kusimamia ubora wa huduma Mamlaka imeendelea kusisitiza na kusimamia matumizi ya tiketi mtandao kwa watoa huduma ya usafiri wa abiria wa masafa marefu.

4) Mamlaka imendelea pia kutoa elimu kwa abiria kuhakikisha wanaposafiri wapatiwe tiketi za mtandao na sio zile za kuandikwa kwa mkono.



*Picha Na. 58: Kituo cha mabasi ya abiria Nanenane- Jiji la Dodoma*

### 2.6.3.3 Udhibiti na Kupunguza ajali.

LATRA imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani katika usimamizi wa huduma za usafiri na usafirishaji mkoani Dodoma ili kuendelea kukabiliana na kupunguza ongezeko la ajali. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kufanya yafuatayo;

1) Kuendelea kufanya ukaguzi wa magari yote yanayotoa huduma ya kusafirishaji wa abiria ili kubaini magari mabovu nakuelekeza yafanyiwe matengenezo ili kukidhi viwango vya ubora.

2) Kusimamia uwepo wa madereva wawili katika mabasi ya masafa marefu.
3) Kuendelea kufuatilia mwenendo wa magari ya abiria kwa kutumia mfumo wa VTS na kuchukua hatua kwa madereva wanaobainika kuendesha magari yao kwa mwendo kasi usioridhisha.
4) Kushirikiana na jeshi la Polisi kikosi cha Usalama barabarani katika kupima ulevi kwa madereva mara kwa mara katika vituo vya mabasi ili kuwabaini madereva wanaoendesha mabasi wakiwa wametumia vileo.
5) Kushirikiana na wadau wote wa usafirishaji ili kuhakikisha ajali zinapungua na ikiwezekana kutokuwepo kabisa.
6) Kuhakikisha vyombo vyote vinavyotoa huduma ya usafiri wa umma vinafuata kanuni za usafirishaji kwa mujibu wa masharti ya leseni.

### 2.6.4 Mawasiliano ya Simu za Mkononi

Mkoa wa Dodoma una Makampuni sita (6) ya mawasiliano. Makampuni hayo ni TTCL, TIGO, VODACOM, AIRTEL, HALOTEL na ZANTEL ambapo wameendelea kutoa huduma katika teknolojia zote za simu yaani 2G, 3G, 4G na 5G. Kuna ongezeko kubwa la vituo vya utoaji huduma za

mawasiliano (Base stations) ikilinganishwa na miaka ya iliyopita.

*Jedwali Na. 11: Idadi ya Vituo kwa Kila Teknolojia*


| **Na** | **Jina la Mtoa Huduma** | **Idadi ya Vituo kwa Kila Teknolojia** | | | **Jumla hadi Desemba 2022** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2G | 3G | 4G | |
| 1 | Airtel | 122 | 96 | 86 | 304 |
| 2 | Halotel | 149 | 66 | 44 | 259 |
| 3 | Tigo | 151 | 135 | 64 | 350 |
| 4 | TTCL | 20 | 24 | 19 | 63 |
| 5 | Vodacom | 142 | 124 | 86 | 352 |
| 6 | Zantel | - | 127 | 40 | 167 |
| 7 | Smile | - | | 4 | 4 |

### 2.6.4.1 Huduma za Matangazo kwa Njia ya Redio

Mkoa wa Dodoma una takribani vituo 27 vinavyorusha matangazo ya redio katika Mkoa wa Dodoma.Vituo 12 kati ya hivyo ni kutoka Mkoa Dodoma (Radio Stations based in Dodoma) kama inavyoonesha kwenye kielelezo hapa chini. Vituo vilivyo baki vinarusha matangazo kutoka nje ya Mkoa lakini vinasikika katika Mkoa wa Dodoma. Mwaka 2022 kituo kipya cha redio (Zabibu FM)

kimefunguliwa wilayani Kongwa na kimepewa kibali pia kurusha matangazo Dodoma mjini.
Katika tangazo la mwaliko wa maombi la mwezi Oktoba 2022, TCRA ilitoa nafasi mbili (2) kwa watoa huduma ambao wanatamani kuwekeza katika huduma za utangazaji kwa njia ya redio mkoani Dodoma.

***Kielelezo Na. 4: Idadi ya Redio zenye Vituo vya kurushia matangazo Dodoma***





### 2.6.4.2 Huduma za Televisheni

### 2.6.4.3 Huduma za Matangazo ya TV kwa Njia ya Waya

Hadi sasa, kuna vituo vya 4 vya TV vinavyorusha matangazo kwa njia ya wire (Cable TV) kama inavyoonesha kwenye kielelezo hapa chini.

*Kielelezo Na. 5: Idadi ya TV kwa njia ya Kebo(Cable TV)*




### 2.6.4.4 Huduma ya TV kwa Njia ya Miundombinu Iliyosimikwa Ardhini (DTT)

Vituo vinavyorusha Matangazo kwa njia ya miundombinu ya ardhini ni vinne (4), kuna kituo kimoja cha televisheni ambacho kimeuheshimisha Mkoa wa Dodoma kwa kurusha matangazo moja kwa moja kutoka mkoa wa Dodoma kupitia king'amuzi cha star-times katika chaneli namba 113. Kituo hiki kinaitwa Dodoma Television.

### 2.6.4.5 Huduma ya TV kwa Njia ya Satelaiti

Huduma za television kwa njia ya Satelaiti kama za Azam, DSTV n.k zinapatikana katika maeneo yote ya Mkoa wa Dodoma pamoja na vijiji vyake

## 2.7 Sekta ya Kilimo, Mifugo na Ushirika

### a. Malengo ya Kilimo

Kila msimu, kupitia Halmashauri, Mkoa unajipangia malengo wa uzalishaji katika kilimo kama mwongozo wa kufuatilia na hatimaye kufanya tathmini ya ufanisi na tija katika uzalishaji ndani ya sekta ya kilimo. Kwa msimu wa mwaka 2022/2023, Mkoa umekisia kuzalisha jumla ya tani 1,231,937 za chakula na tani 567,314 za mazao ya biashara.

***Jedwali Na. 12: Malengo ya Uzalishaji kwa Msimu wa 2022/2023***

| **Halmashauri** | **Malengo ya uzalishaji** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Eneo (Ha)** | **Eneo (Ha)** | **Uzalishaji (Tani)** | **Uzalishaji (Tani)** |
| | **Mazao ya Chakula** | **Mazao ya Biashara** | **Mazao ya Chakula** | **Mazao ya Biashara** |
| Bahi | 84,039 | 66,985 | 145,718 | 83,067 |
| Chamwino | 154,685 | 108,449 | 136,792 | 110,076 |
| Chemba | 122,120 | 55,171 | 195,251 | 61,845 |
| Dodoma Jiji | 25,150 | 12,942 | 47,651 | 30,888 |
| Kondoa | 75,230 | 76,347 | 120,150 | 89,863.00 |
| Kondoa Mji | 20,880.00 | 11,432 | 17,814.50 | 14,965.4 |
| Kongwa | 198,671.80 | 111,347.40 | 432,905.80 | 121,735.90 |
| Mpwapwa | 91,602 | 48,275 | 135,655 | 54,874.00 |
| **Jumla** | **772,377.60** | **490,948.4** | **1,231,937.30** | **567,314.3** |

**b.** Mahitaji ya Chakula Msimu wa 2023/2024

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, mkoa wa Dodoma una jumla ya watu 3,085,625

ambao wanahitaji chakula cha wanga kipatacho tani 732,065 kwa mwaka; huu ni wastani wa tani moja kwa kila kaya kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini

***Jedwali Na. 13: Makisio ya Mahitaji ya Chakula kwa msimu wa 2023/2024***

| . | **Wilaya** | **Idadi ya Watu** | **Idadi ya Kaya** | **Ukubwa wa Kaya** | **Mahitaji ya chakula (Tani)** | **Wastani wa Mahitaji ya chakula kwa kila kaya (Tani)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kondoa | 325297 | 73073 | 4.5 | 77,177 | 1 |
| 2 | Mpwapwa | 403247 | 99004 | 4.1 | 95,670 | 1 |
| 3 | Kongwa | 443867 | 101761 | 4.4 | 105,307 | 1 |
| 4 | Chamwino | 486176 | 118812 | 4.1 | 115,345 | 1 |
| 5 | Dodoma | 765179 | 214331 | 3.6 | 181,539 | 1 |
| 6 | Bahi | 322526 | 75792 | 4.3 | 76,519 | 1 |
| 7 | Chemba | 339333 | 75050 | 4.5 | 80,507 | 1 |
| | **Total** | **3,085,625** | **757,823** | | 732,065 | |

i. kukidhi mahitaji mengine ya kiuchumi

Baadhi ya mazao ya kimkakati kwa usalama wa chakula na kiuchumi katika mkoa wa Dodoma ni kama ifuatavyo hapa chini:-

**c. Zao la Mtama**

Kupitia wadau mbalimbali, takwimu za uzalishaji wa zao la Mtama ndani ya miaka miwili zinaonyesha kuwa;

a) Uzalishaji wa Mtama kwa ujumla umeongezeka kutoka tani 32,178 mwaka 2021 hadi tani 61,098 2022.
b) Idadi ya wakulima waliotumia Mbegu bora ya Mtama waliongezeka kutoka 11,715 Mwaka 2021 hadi wakulima 20,366
c) Kupitia uratibu wa Masoko ya zao la Mtama, tathmini ya mauzo ya zao la Mtama yalipanda kutoka Shilingi 1.8 Bilioni Mwaka 2021 hadi Shilingi. 2.3 Bilioni Mwaka 2022.

**d. Zao la Alizeti**

a) Kupitia Mikakati na hamasa ya Serikali, wadau na wananchi kwa ujumla, uzalishaji wa zao la Alizeti katika Mkoa wa Dodoma ulipanda kutoka tani 190,000 katika Mwaka 2021 hadi tani 267,627 Mwaka 2022
b) Uzalishaji huu ulipunguza bei ya Mafuta ya kula ya Mlizeti kutoka Shilingi 6,500 – 7,000 kwa lita Desemba, 2021 hadi Shilingi 4,000 – 4,500 kwa lita Mwezi Desemba, 2022.

**e. Zao la Zabibu**

Katika kipindi cha Miaka Miwili, Zabibu iliingizwa kwenye orodha ya Mazao ya

kimkakati ya serikali na hivyo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassimu Majaliwa (Mb) kufanya ziara mahsusi kwa ajili ya zao hili.



*Picha Na. 59: Zao la zabibu Chinangali II, Chamwino*

### 2.7.1.1 Ruzuku za Pembejeo za Kilimo

**a. Mbolea ya Ruzuku**

Jumla ya Wakulima 2032 wenye jumla ya ekari 11,367 wamenunua Mbolea ya Ruzuku jumla ya Mifuko 7,189 (sawa na tani 359.45)

**b.** Mbegu za Alizeti

Jumla ya tani 24 za Mbegu za Alizeti za Ruzuku zimenunuliwa hadi Desemba, 2022. Zoezi hili linaendelea




*Picha Na. 60: Ruzuku ya Mbegu za Alizeti*

**c. Uboreshaji wa Huduma za Ugani**

Mwaka 2022, Mkoa wa Dodoma ulipokea jumla ya Pikipiki 264 kwa ajili ya Maafisa Ugani wote ndani ya Mkoa. Pikipiki hizi zimesaidia kuongeza utoaji wa huduma za ugani.



*Picha Na. 61: Ugawaji wa Pikipiki*

d. **Kilimo cha Umwagiliaji**

Ili kuwa na uhakika na kilimo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inajenga Miradi (Skimu) mbalimbali za umwagiliaji katika Mkoa wa Dodoma. Zifuatazo ni skimu zinazojengwa mkoa wa Dodoma.

i. Bwawa la Umwagiliaji la Msagali, Mpwapwa – Shilingi 27 Bilioni. Uwezo wa Bwawa ni kuchukua lita 92 Bilioni na litakuwa na uwezo wa kumwagilia zaidi ya Ekari 20,000 kwa Mwaka.



***Picha Na. 62 Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliji Msagali.***

ii. Bwawa la Membe, Chamwino – 10.9 Bilioni Uwezo wa kutunza lita 12 Bilioni na kumwagilia Ekari 8000 kwa Mwaka.



*Picha Na. 63 Bwawa la Membe, Chamwino*

**e. Mradi wa Building Better Tomorrow (BBT)**

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanziasha Mradi wa Building Better Tomorrow ambao unahusisha kilimo cha maeneo makubwa nchini (block farms). Dodoma ina jumla ya Ekari 11,000 katika kijiji cha Ndogoye, Chamwino na 2700 kijiji cha Ikumbulu, Bahi, Shamba la ekari 11 katika Kijiji cha Ndogoye pamoja na Mitambo ya kulisafisha

### 2.7.2 Sekta ya Mifugo

i. Uongezekaji wa Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo.Kwa Mwaka 2021/2022 hadi 2022/2023,Uzalishaji wa Mazao ya Nyama ya Ng'ombe,Mbuzi,Kondoo,Kuku umeongezeka kutoka Nyama tani 6410 hadi Nyama tani 7223 na Uzalishaji wa Ngozi umeongezeka kutoka vipande 63122 hadi vipande 64727kama inavyoonekana katika Jedwali .

*Jedwali Na.13: Mazao ya Nyama*

| **Mazao ya Nyama kwa Tani** | **2021/2022** | **2022/2023** |
|---|---|---|
| Nyama ya Ng'ombe | 4,522 | 5,565 |
| Nyama ya Mbuzi | 725 | 801 |
| Nyama ya Kondoo | 195 | 205 |
| Nyama ya Nguruwe | 674 | 300 |
| Nyama ya Kuku | 294 | 355 |
| **Jumla** | **6410** | **7223** |
| **Mazao ya Ngozi kwa vipande** | | |
| Vipande vya Ngozi ya Ng'ombe | 62,032 | 63,421 |
| Vipande vya Ngozi ya Mbuzi | 778 | 865 |
| Vipande vya ngozi ya Kondoo | 312 | 441 |
| **Jumla** | **63122** | **64727** |

a. **Ujenzi na Ukarabati wa Majosho**
Jumla ya Majosho 40 yamejengwa (14 yamekamilika, 26 ujenzi unaendelea) Kwa gharama ya Tshs 685,100,000/= fedha kutoka Serikali kuu, 14,000,000/=mapato ya Halmashauri na 29,000,000 ni nguvu za wananchi.

*Jedwali Na.14: Ujenzi na Ukarabati wa Majosho Kiwilaya;*

| Wilaya | Majosho Mapya yaliyojengwa | Mapya yaliyokamilika | Yaliyokarabatiwa | Fedha zilizotolewa na Serikali Kuu | Fedha za Ndani za Ukarabati |
|---|---|---|---|---|---|
| Mpwapwa | 12 | 3 | | 183,600,000 | |
| Bahi | 10 | 0 | | 180,000,000 | |
| Chamwino | 9 | 4 | | 162,000,000 | |
| Kongwa | 3 | 4 | | 72,000,000 | |
| Chemba | 5 | 3 | 3 | 87,000,000 | 14,000,000 |
| **Jumla** | **40** | **14** | **3** | **685,100,000** | **14,000,000** |

**b.** Kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa za ruzuku na uogeshaji wa mifugo Mkoani na hivyo kusababisha magonjwa ya mifugo yasababishwayo na kupe,mainzi pamoja na mbu kupungua kwa asilimia 44.

**c.** Uchimbaji wa Malambo na Ujenzi wa Makaro ya kunyweshea mifugo maji

Malambo ya 4 ya kunyweshea mifugo Maji yamechimbwa katika Wilaya ya Chemba (3) na

Mpwapwa(1) kwa thamani ya Tshs 807,000,000/=.

## 2.8 UWEKEZAJI VIWANDA NA BIASHARA

Mkoa unaendelea kuwezesha ukuaji wa Sekta ya Uwekezaji Viwanda na Biashara na kupata mafanikio yafuatayo;

### a. Utengaji wa maeneo ya Uwekezaji

Mkoa umetenga maeneo yenye ukubwa wa Hekta 16,197.59 kwa ajili ya uwekezaji katika Halmashuri zote kama ifuatavyo;

***Jedwali Na. 17 Maeneo ya Uwekezaji***

| Na | Halmashauri | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|
| 1. | Bahi | 20.9 |
| 2. | Chamwino | 145.88 |
| 3. | Chemba | 39.25 |
| 4. | Dodoma Jiji | 15,437.6 |
| 5. | Kondoa | 164.8 |
| 6. | Kondoa Mji | 40 |
| 7. | Kongwa | 233.2 |
| 8. | Mpwapwa | 115.96 |
| | **Jumla** | **16,197.59** |

Maeneo hayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, makazi, maduka makubwa ya biashara, burudani, taasisi za elimu na afya, masoko,

(i) Viwanda
(ii) Biashara
(iii) Viwanja vya michezo (golf course, play fields,
(iv) Maeneo ya burudani (Parks Maduka makubwa (Shopping malls, super markets, shops
(v) Uendelezajimiliki (Hotels and apartment)
(vi) Eneo maalum la kiuchumi (Economic Processing Zone (EPZ)
(vii) Warehouses, godowns

**b. Maendeleo ya viwanda**

Mkoa unaendelea kuratibu maendeleo ya viwanda na kuwezesha kuwa na kumla ya viwanda **2,943** kwa mchanganuo wa 8 vikubwa, 13 vya kati na 2922 vidogo.

***Jedwali Na. 16: Aina ya bidhaa zinazozalishwa***

| Na | Bidhaa | Vikubwa | Vya Kati | Vidogo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Alizeti | | 5 | 509 | 514 |
| 2 | Unga | 1 | 2 | 1588 | 1591 |
| 3 | Magodoro | 1 | | | 1 |
| 4 | Kokoto | 2 | | | 2 |
| 5 | Mbolea | 1 | | | 1 |
| 6 | Mvinyo | 2 | 2 | 37 | 41 |
| 7 | Nyama | 1 | | | 1 |
| 8 | Samani | | | 80 | 80 |
| 9 | Mikate | | | 40 | 40 |
| 10 | Alminium | | | 49 | 49 |
| 11 | Mabati | | 2 | | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | Karanga | | 2 | 12 | 14 |
| 13 | Kuchapisha | | | 16 | 16 |
| 14 | Kuchomelea | | | 48 | 48 |
| 15 | Kusaga chupa | | | 1 | 1 |
| 16 | Kushona | | | 205 | 205 |
| 17 | Chumvi | | | 32 | 32 |
| 18 | Maji | | | 8 | 8 |
| 19 | Matofali | | | 236 | 236 |
| 20 | Maziwa | | | 1 | 1 |
| 21 | Mbao | | | 57 | 57 |
| 22 | Misumari | | | 1 | 1 |
| 23 | Ngozi | | | 2 | 2 |
| | **Jumla** | **8** | **13** | **2,922** | **2,943** |

c. **Uendelezaji wa viwanda vidogo**

Yafuatayo yamefanyika katika kuendeleza viwanda vidogo;

(i) Viwanda vipya 48 (Vidogo- 47 na Kati -1) vimeanzishwa.
(ii) Kusambazaji teknolojia mpya 22 katika Nyanja za Zabibu, Karanga, Mtama, Mahindi, Alizeti na Tofali na mazao mengine.
(iii) Wanaviwanda na wajasiliamali 1,753 wamepewa mafunzo ya namna ya kuboresha mazingira ya uzalishaji na uanzishwaji wa viwanda na biashara.


(iv) Wajasiriamali 52 wamepata bure nembo ya ubora wa bidhaa kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

d. **Ujenzi** wa masoko

(i) Ujenzi wa Soko la kisasa (Machinga Complex) uliogharimu Shilingi **9,529,747,200.66 (Shilingi 6,529,747,200.66** mapato ya ndani, Shilingi **2,500,000.00** ruzuku toka Serikali kuu na Shilingi **500,000,000.00** Mradi wa TCRP)



***Picha Na. 64 NaUjenzi wa Soko la Machinga (Machinga Complex) – Dodoma Jiji***



***Picha Na. 65 Wafanyabiashara wakifanya biashara katika soko la Machinga (Machinga Complex) – Dodoma Jiji***

## 2.9 Shirika la Nyumba la Taifa Mkoa wa Dodoma.

### 2.9.1 Mafanio ya Shirika la Nyumba(NHC) Mkoa wa Dodoma

**a.** Shirika limefanikiwa kujenga na kuuza nyumba 300 katika eneo la Iyumbu kama inavyonekana kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 17: Nyumba zilizojegwa**

| Maelezo | Idadi | Gharama | Vat | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Nyumba zilizouzwa | 78 | 11,418,694,524.53 | 2,055,365,014.41 | 13,409,522,475.97 |
| Nyumba zilizobaki | 222 | 11,225,246,527.00 | 2,020,544,374.86 | 13,310,327,964.83 |
| **Jumla** | **300** | **22,643,941,051.53** | **4,075,909,389.27** | **26,719,850,440.80** |



*Picha Na. 66 Nyumba za Makazi Iyumbu*



*Picha Na.67 Nyumba za Makazi Iyumbu*

b. Shirika limefanikiwa Kujenga Majengo 8 ya Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba yenye thamani ya Shilingi bilioni 186.



*Picha Na 68 Majengo ya Wizara ya Utamaduni Mtumba*



*Picha Na 69 Majengo ya Wizara Viwanda Mtumba*

c. Shirika limekuwa likishauri Wizara mbili katika ujenzi wa Majengo yao ambayo ni Wizara ya Fedha na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

## 2.10 Wakala Wa Majengo Tanzania (TBA) Utangulizi

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya 1997 kutokana na iliyokuwa Idara ya Majengo ya Wizara ya Ujenzi. Wakala ulizinduliwa rasmi tarehe 17 Mei 2002 kwa madhumuni ya kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa kutumia njia za kibiashara na uongozi bora wa fedha ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) unayo majukumu ya kutoa Huduma za Miliki (kuipatia makazi Serikali na Watumishi wa Umma), ushauri na ujenzi.

### 2.10.1 Miradi Inayotekelezwa Dodoma

#### 2.10.1.1 Miradi ya Kimkakati

a) **Ujenzi wa Nyumba 3500 za makazi ya Watumishi wa Umma katika eneo la Nzuguni.**

Mradi huu upo katika eneo la Nzuguni B lenye jumla ya ekari 630. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa nyumba za kawaida, ujenzi wa maghorofa, Soko, Kituo cha Polisi, Shule, eneo la michezo, pamoja na eneo la ibada yaani Msikiti na Kanisa.

Kazi zote za usanifu na Ujenzi zinafanywa na Wakala wa majengo Tanzania kwa kutumia Wataalam wake wenyewe. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa kutekeleza mradi huu ni Tshs 14, 373, 270, 000 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya Ujenzi wa awamu hii ya kwanza uliohusisha ujenzi wa nyumba 150 zenye mita za mraba 101 kwa kila nyumba.

Ujenzi huu ulianza rasmi mnamo tarehe 25/03/2022 na unatarajiwa kukamilka ifikapo tarehe 31/3/2023. Hatua za utekelezaji kwa awamu hii ya kwanza umefikia asilimia 85%.
Aidha Ujenzi wa awamu ya pili wa nyumba 150 nyingine umekwisha anza na unatarajiwa kukamilika mapema 2024.



*Picha Na. 70: Nyumba za kupanga*

**b) Ujenzi wa Nyumba 20 za Watumishi katika eneo la Kisasa**

Serikali imetoa fedha kiasi cha Shilingi 5,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kiasi cha Tsh. 2,000,000,000.00 kwa mwaka fedha 2021/2022 kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba ishirini (20) za Watumishi wa Umma katika eneo la Kisasa/Mwangaza Jijini Dodoma. Ujenzi wa nyumba hizi unahusisha nyumba kubwa (main houses) yenye eneo la mita za mraba 203.5, nyumba za wahudumu/wafanyakazi (servant quarters) zenye mita za mraba 26.18 kila moja pamoja na ujenzi wa kibanda cha mlinzi chenye mita za mraba 8.3. Pia mradi huu umehusisha ujenzi wa uzio wa matofali kwa kila nyumba pamoja na mandhari ya nje.

Mradi huu umekamilika na nyumba hizi zimepangishwa na hivyo kupelekea Serikali kuanza kukusanya mapato kwa njia ya kodi.



*Picha Na. 71: Nyumba 20 zilizojengwa Kisasa*

c) **Ujenzi wa Mji wa Kiserikali Mtumba ( Magufuli City).**

Ili kutimiza adhima ya serikali kuhamia Dodoma, Wakala wa Majengo ulipewa jukumu la kufanya usanifu wa mji huu wa kiserikali. Utekelezaji wa kazi hii ulifanywa kwa kutumia wataalam wake wa ndani ambapo Wakala uliandaa michoro,gharama pamoja na kufanya usimamizi wa ujenzi wa kazi hizo chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Uratibu na Bunge ambaye ndie mratibu mkuu wa shughuli za serikali kuhamia Dodoma.

Utekelezaji wa kazi hii unaendelea na Wakala una jukumu la kusimamaia majengo ya ofisi za Wizara 17 na Tassisi moja ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo moja la Ofisi Rais Utumishi na Utawala Bora. Gharama ya fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa kazi hizi ni jumla ya kiasi cha Tsh **386,186,396,646.58** na utekelezaji wake ulianza rasmi tarehe 21 Septemba 2021 na kutarajia kukamilika tarehe 20 Machi 2025.
Hadi kufikia sasa utekelezaji wa kazi hii umefikia asilimia 60 (60%).



***Picha Na. 72: Jengo la Utumishi na Utawala bora linalojengwa na TBA katika mji wa kiserikali (Magufuli City)***

### 2.10.1.2 Miradi ya Ushauri

Serikali kupitia TBA inalo jukumu la Kusimamia miradi ya ujenzi na kutoa huduma ya ushauri kwa Majengo ya Serikali pamoja na ushauri wowote unaohusu majenzi Serikalini.

Katika kutekeleza agizo la Serikali kuhamia Dodoma, Serikali ya Awamu ya Sita ilitenga fedha kupitia Wizara na Taasisi mbalimbali ili kuziwezesha kujenga ofisi zao jijini Dodoma. Katika kufanikisha adhma hiyo, Wakala umeingia mikataba ya Ushauri na Usimamizi na Taasisi mbalimbali ili kuwezesha ujenzi wa ofisi zao kukamilika mapema na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa watumishi husika jijini Dodoma. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;


a) Ukarabati wa jengo la maabara katika hospitali ya Benjamini Mkapa,
b) Ujenzi wa jengo la mionzi na kitengo cha kansa katika Hospitali ya Benjamini Mkapa,
c) Ujenzi wa jengo la huduma za upandikizaji wa Figo katika hospitali ya Benjamini Mkapa,
d) Ujenzi wa jengo la ofisi za REA,
e) Ujenzi wa jengo la ofisi TARI,
f) Ujenzi wa jengo la ofisi TEMESA katika eneo la NCC Link Dodoma,
g) Ujenzi wa jengo la ofisi la Tume ya Uchimbaji madini,
h) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS),
i) TBA inasimamia ujenzi wa Jengo la PPRA,
j) Ukarabati wa nyumba za Watumishi Kisasa, Area D na Kikuyu flats.


## 2.11 Sekta ya Nishati na Umeme

### 2.11.1 TANESCO

**Mafanikio katika Sekta ya Umeme Mkoa wa Dodoma kwa kipindi cha miaka miwili ni kama ifuatavyo:**

1) Upanuzi wa Kituo cha Grid cha kupooza umeme cha Zuzu kutoka Megawati 48 mwaka 2020 hadi Megawati 200 mwaka 2022 wenye thamani ya Shilingi Bilioni 53. Upanuzi huu umeboresha huduma ya upatikanaji wa umeme Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Gairo Mkoa wa Morogoro na hivyo kuepusha mgao wa umeme wa saa 24 ambao ungejitokeza endapo upanuzi usingefanyika.






**B: Upanunuzi wa kituo cha kupooza Umeme cha Mzakwe kutoka Megawati 8 (MVA 10) mwaka 2021 hadi Megawati 20 (MVA 25) mwaka 2022 wenye thamani ya Shilingi bilioni 3.4.**

Kituo hiki kinapoza umeme kwa ajili ya visima vya maji vya DUWASA na kutoa huduma kwa Wananchi wa Mndemu-Wilaya ya Bahi. Upanuzi huu wa kuongeza transfoma umeleta ufanisi mkubwa wa kituo kuwa na mbadala endapo transfoma moja ikipata hitilafu.

**C: Mradi wa kupeleka umeme eneo la Viwanda Km 25.5 ili kuboresha upatikanaji wa umeme wenye thamani ya Shilingi bilioni 2.6.**

Eneo la viwanda Nala halikuwa na umeme wa uhakika na hivyo wawekezaji wengi kutovutiwa kuwekeza eneo hilo. Mradi huu utahudumia Kiwanda cha mbolea Intracom na viwanda vingine vitakavyojengwa na wawekezaji.

## D: Kusambaza miradi ya umeme Vijijini (REA) yenye thamani ya Shilingi bilioni 201.9

Katika kipindi cha miaka miwili 2021/2022 hadi 2022/23 Serikali imetekeleza miradi minne ya usambazaji wa umeme Vijijini kwa ujumla kama ifuatavyo: -

*Jedwali Na. 19 Miradi ya Umeme Vijijini*

| Urefu wa njia kubwa zilizojengwa (Kwa kilometa) | Urefu wa njia Ndogo zilizojengwa (LV lines) kwa Kilometa | Idadi ya Transfoma zilizofungwa kwa wananchi | Maunganisho ya mwanzo |
|---|---|---|---|
| 2,641 | 3,627.03 | 807 | 63,513 |

Mpango wa kusambaza umeme vijijini unaoendelea (REA awamu ya Tatu mzunguko wa pili) una lengo la kuvifikia vijiji 114 vilivyosalia katika Mkoa wetu hivyo kufikia Mwezi wa Machi 2023 kulingana na Mkataba wa Wakandarasi wanaotekeleza Mradi huu, hakuna Kijiji cha Mkoa wa Dodoma ambacho kitakuwa hakina umeme.

## E: Maboresho katika eneo la Huduma kwa Mteja

### E.1 Kuanzishwa kwa Mfumo wa Nihudumie:

TANESCO Mkoa ilijiunga na Kituo cha Miito ya simu cha pamoja (Unified Call Centre) Mwezi Julai 2022. Mteja kokote aliko ndani ya Mkoa hahitaji tena kuja

kwenye ofisi za TANESCO ili apate huduma anayohitaji, anapiga namba **0748550000** na kupewa tiketi namba ya tatizo lake.

Tiketi hiyo inatumwa moja kwa moja kwenye Kiunga (Service centre iliyokaribu naye ili ahudumiwe kwa haraka. Wafanyakazi  wa Tanesco hupimwa kwa idadi ya tiketi anazohudumia kwa siku na kwa muda gani.

**E.2 Mfumo wa Nikonnekti:**

Lengo la kuanzishwa kwa mfumo huu ni kuondoa kero mbalimbali zilizokuwa zinajitokeza kwa mteja katika safari ya kupata huduma ya Umeme. Vilevile, mfumo huu unaweka usimamizi madhubuti wa Maunganisho ya mteja toka anajaza fomu hadi kuunganishiwa. Maombi yaliyopokelewa katika Mkoa kuanzia Julai 2022 hadi Januari 15, 2023 ni maombi 45,369 Kwa njia mbalimbali.

Takwimu zinaonesha kuwa wananchi waliofika ofisini ni asilimia 7.8 tu ya idadi hiyo. Jumla ya wateja 36,480 waliweza kuunganishwa sawa na asilimia 80.4 kwa wastani wa siku 6.

**Jedwali Na. 20 Wateja waliounganishiwa Umeme**

| Halmashauri | Online (web) | Physical Visit | Ussd (*152*00#) | Mobile app (simu) | Jumla ya maombi katika Wilaya | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bahi | 1035 | 148 | 637 | 516 | 2336 | 6.3 |
| Chamwino | 3873 | 501 | 335 | 628 | 5337 | 9.4 |
| Chemba | 2204 | 348 | 178 | 472 | 3202 | 10.9 |
| Dodoma | 18591 | 262 | 1471 | 3621 | 23,945 | 1.1 |
| Kondoa | 2083 | 140 | 299 | 355 | 2877 | 4.9 |
| Kongwa | 1177 | 115 | 1836 | 1466 | 4594 | 2.5 |
| Mpwapwa | 1051 | 599 | 857 | 571 | 3078 | 19.5 |
| **JUMLA** | **30,014** | **2,113** | **5,613** | **7,629** | **45,369** | **7.8** |

## F: Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23

Katika mwaka wa fedha huu 2022/23 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi 24,034,612,733 kwa ajili ya ujenzi wa Miradi mipya kuwafikishia huduma ya umeme wananchi, uboreshaji wa Huduma iliyopo katika baadhi ya maeneo, ununuzi wa vifaa vya Maunganisho ya wateja pamoja na ukarabati wa miundombinu ya umeme kama ifuatavyo:

*Jedwali Na. 21 Bajeti iliyotengwa mwaka 2022/23*

| **Kifungu cha fedha** | **Bajeti iliyotengwa** | **Kiasi kilichotumika hadi Disemba 2022** | **Asilimia ya Matumizi** |
|---|---|---|---|
| Vifaa kwa ajili ya Maunganisho ya Umeme (Ujenzi wa Service Lines) | 6,465,697,845 | 6,465,697,845 | 100% |
| Miradi ya Matengenezo ya Miundombinu (Maintenance) | 5,394,627,532 | 4,051,703,411 | 75% |
| Mradi ya Kuongeza miundombinu ya umeme (New Extension Projects) | 6,567,627,763 | 3,316,431,484 | 50% |
| Ukamilishaji wa Miradi inayoendelea (Ongoing projects) | 126,133,424 | 126,133,424 | 100% |
| Miradi ya Uboreshaji Miundombinu ya Umeme (Voltage Improvement Projects) | 5,480,526,169 | 3,732,267,196 | 68% |

## 2.12 Wakala wa Vipimo (WMA)

Wakala wa Vipimo ni taasisi ya serikali iliyo chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, iliyopewa jukumu la kumlinda mlajji kupitia matumizi ya Vipimo sahihi vinavyotumika katika sekta ya Biashara, Afya, Usalama na Mazingira. Wakala wa vipimo inatekeleza majukumu yake chini ya sheria ya Vipimo Sura 340 (mapitio ya 2002). Mafanikio ya Wakala ni kama ifuatayo:

a. Kufanya ukaguzi na uthibiti wa vipimo vya aina mbalimbali, kaguzi za kushitukiza, utoaji wa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya vipimo kwenye vituo vya ukaguzi, Elimu kwa Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Kongwa na utoaji wa elimu kwa wauzaji wa gesi juu ya matumizi ya mizani ili kuhakikisha uzito wa mitungi ya gesi inayouzwa upo sahihi.

b. Vipimo 20,820 vilikaguliwa ikilinganishwa na lengo la kukagua vipimo 13,154 kwa mwaka 2022/2023**.** Aidha kati ya vipimo hivyo Wakala wa vipimo ilihakiki vipimo vya miradi ya mkakati zikiwemo dira za maji 14,191 kati ya 6623 zilizokadiriwa ambazo ni za mamlaka za maji za **DUWASA, KONDUWASA, MPWUWSA, KIBAWASA** na **MBEYAUWASA.**

c. Kukusanya jumla ya Tsh. 464, 940, 151.00 ikilinganishwa na Tsh. 398, 410, 100.00 **z**ilizokuwa zimekadiriwa kwa kipindi cha Julai

hadi Desemba mwaka 2022/2023, hivyo kuvuka lengo kwa kiasi cha shilingi 66, 498, 051.26.

## 2.13 TANAPA

## 2.14 Mafanikio Yaliyopatikana Katika Utalii

### a. Kutangaza Vivutio Vya Utalii Ndani na Nje ya Nchi

Katika Kipindi Cha Uongozi wa Raisi wa awamu ya Sita Mhemimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania limeendelea kuhamasisha Utalii ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa utalli ili kuongeza watalii kutoka 1,500,000 hadi kufikia watalii 5,000,000 na kukusanya mapato yatokanayo na utalii kiasi cha Dola za Kimarekani Billion 6 ifikapo mwaka 2025/26,

Shirika kwa kushirikiana na wadau wengine wa utalii limeendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kutumia mitandao ya kijamii, kama vile Twitter, WhatsApp, Instagram, YouTube, Facebook na Tiktok, na kushiriki katika Maonyesho ya Kimataifa, Makongamano na Road Shows pamoja na kushirikiana na Balozi za Tanzania nje ya nchi.

### b. Utalii kuimarika Baada ya Janga la Uviko 19

Katika Kipindi cha Uongozi wa Raisi wa Awamu ya Sita, ni Kipindi ambacho Dunia ilipita katika kipindi cha changamoto ya athari kubwa ya janga la

UVIKO-19 na hivyo kusababisha kupungua kwa watalii kwa kiasi kikubwa. Katika jitihada za kukuza utalii hasa baada ya janga la UVIKO-19 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliandaa na kuzindua Filamu ya ***Tanzania: The Royal Tour***. Na mafanikio makubwa yameonekana baada ya kuzindua Filamu hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 hali ya utalii ilianza kuimarika ukilinganisha na mwaka wa fedha wa 2020/2021. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 jumla ya watalii 1,053,701 walitembelea Hifadhi za Taifa Tanzania ikiwa ni aongezeko la Watalii 551,759 ukilinganisha na mwaka 2020/2021.

**c. Kuboresha Miundombinu na Huduma na za Utalii**

Shirika limeendelea kuboresha huduma na miundombinu ya watalii katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Tanzania, ikiwa ni pamoja na kufungua miundo mbinu ya Barabara, Viwanja vya ndege na kuboresha malazi ya watalii kama inavyoainishwa hapa chini;

i. Kupitia Mradi wa TCRP Shirika linakarabati barabara zenye urefu wa kilomita 1,552 na njia za kupanda mlimani kilomita 21.6. Shirika pia limekarabati kilomita 3,750 na kilomita 178 za njia za kupanda mlimani kupitia bajeti ya kawaida katika mwaka fedha 2021/2022 katika Hifadhi za Tarangire na Hifadhi nyinginezo.

ii. Kununua seti mpya 4 za mitambo.mashine na malori ya kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, majengo ya huduma za kitalii katika hifadhi za Taifa Tanzania.
iii. Kukarabati viwanja vya ndege 5 kupitia mradi wa TCRP na viwanja 24 kupitia bajeti ya kawaida kwa kuboresha uwanja, kujenga miundombinu ya vyoo, sehemu za kupumzikia watalii (waiting lounges) katika Hifadhi za Taifa Tanzania.
iv. Kujenga miundombinu ya ukusanyaji mapato (Revenue collection centres) mpya 3 kupitia mradi wa TCRP katika Hifadhi za Taifa ikiwemo hifadhi ya Taifa Tarangire

**d. Maboresho ya Mifumo ya Sayansi na Teknolojia**

Kutumia sayansi na teknolojia katika kuimarisha shughuli za uhifadhi na utalii hali hii imeboresha mazingira katika huduma bora kwa watalii ikilinganishwa na zamani. Pia imesaidia sana katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato.

**e. Kutangaza Fursa za Uwekezaji katika Hifadhi za Taifa Tanzania**

Kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Hifadhi za Taifa Tanzania na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya shughuli na huduma za utalii.

Katika kipindi husika, Shirika limeainisha maeneo 110 ya uwekezaji yenye uwezo wa vitanda 5,500 kulingana na Mpango wa Ujumla wa Uendeshaji wa kila Hifadhi ya Taifa Tanzania (General Management Plan).

Shirika litaendelea kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi na umma ili kuwekeza katika maeneo ya hifadhi kwa lengo la kuongeza idadi ya vitanda na kupanua wigo wa ukusanyaji mapato. Vilevile kutangaza vivutio na fursa za uwekezaji kwa kutumia mitandao ya kijamii kama vile maonesho ya kitaifa na kimataifa, Twitter, Facebook, Instagram na Tovuti ya Shirika.

**f. Shirika limepokea cheti ubora wa utoaji wa huduma Mbalimbali za Kimataifa**

Kutokana na juhudi za utangazaji, Hifadhi za Taifa Tanzania zimeweza kujulikana Dunia nzima na Shirika limepata tuzo zifuatazo;

i. Shirika limepokea cheti cha utoaji wa huduma kwa kuzingatia viwango vya ubora kimataifa (ISO 9001:2015) ambapo Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Mkomazi, Arusha, Tarangire na Ziwa Manyara, Kanda ya Kaskazini na Makao Makuu ya shirika zilitunukiwa tuzo hiyo baada ya kukidhi vigezo husika.

ii. Tuzo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa Hifadhi Bora Barani Afrika kwa 2022. Tuzo hii hutolewa na Shirika la "World Travel Awards" la nchini Uingereza ambapo hii ni mara ya ***nne mfululizo*** kwa hifadhi hii kushinda tuzo hiyo tangu mwaka 2019.

iii. Tuzo ya utoaji huduma kwa ubora ijulikanayo kama "Best Practice Award - Diamond Category for 2022" iliyotolewa na Taasisi ya "European Society for Quality Research (ESQR)". Tuzo hizo za utoaji wa huduma bora hutolewa kila mwaka na taasisi hiyo ya ESQR kwa kutambua taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali pamoja na watu binafsi wanaotoa huduma za viwango vya juu. Hii ni mara ya tatu kwa Shirika kupata tuzo kama hii ambapo pia katika mwaka 2020 (Gold Category) na mwaka 2021 (Platinum Category) zilitolewa.

## 2.15 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

### 2.15.1 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

Mafao Yanayotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

i. Huduma za matibabu
ii. Malipo ya ulemavu wa muda
iii. Malipo ya ulemavu wa kudumu
iv. Malipo kwa anayemhudumia mgonjwa
v. Huduma ya ukarabati naushauri nasaha

vi. Malipo kwa wategemezi endapo mfanyakazi atafariki
vii. Gharama za mazishi

***Jedwali Na. 22 Madai yaliyopokelewa Mkoa wa Dodoma (Julai-Desemba)***

| S/N | Mwaka /Kipindi | Madai Yaliyopokelewa |
|---|---|---|
| 1 | 2019/2020 | 72 |
| 2 | 2020/2021 | 39 |
| 3 | 2021/2022 | 79 |
| 4 | 2022/2023 | 101 |

## 3.0 MIPANGO YA MKOA KWA MWAKA 2023/24-2025/26

### 3.1 Malengo ya Ukusanyaji Mapato ya Halmashauri

i. Kuongeza ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri kutoka Shilingi **72,717,906,610** mwaka 2022/23 hadi Shilingi 84,966,510,799 mwaka 2025/26.
ii. Kuongeza fedha za miradi ya maendeleo kwa kigezo cha 40% na 60% za Mapato ya ndani ya Halmashauri kutoka Shilingi **35,053,432,677** mwaka 2022/23 hadi Shilingi **28,598,742,718 mwaka** 2025/26.
iii. Kuongeza fedha za mikopo ya Wanawake, Vijana na walemavu (10%) za Mapato ya ndani

ya Halmashauri kutoka Shilingi **5,581,221,000** mwaka 2022/23 hadi Shilingi **7,188,112,587** mwaka 2025/26.

**3.2 Malengo ya Seksheni ya Elimu**

i. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la awali kutoka 72,927 mwaka 2022/23 hadi 85889 ifikapo 2025/26
ii. Kuongeza uandikisha wa wanafunzi wa darasa la kwanza kutoka 90,301 mwaka 2022/23 hadi 97457 ifikapo 2025
iii. Kuongeza ufaulu wa darasa la saba asilimia 83.01 mwaka 2022 hadi asilimia 96 ifikapo 2025.
iv. Kuongeza Ujenzi wa vyumba vya madarasa kutoka 6,205 mwaka 2022 hadi 7826 ifikapo 2025.
v. Kuongeza madawati kutoka 110426 mwaka 2022 hadi 118544 ifikapo 2025.
vi. Kuongeza ufaulu wa kidato cha nne kutoka asilimia 88 mwaka 2022 hadi asilimia 98 ifikapo 2025.
vii. Kuongeza Ujenzi wa vyumba vya maabara kutoka 175 mwaka 2022 hadi 423 ifikapo 2025.
viii. Kuongeza viti na meza za wanafunzi kutoka 92421 mwaka 2022 hadi 113,200 ifikapo 2025.

**3.3 Malengo yaliyowekwa kwa ajili ya kuimarisha sekta ya Afya mwaka 2022/2023 hadi 2025/26**

i. Kuongeza idadi ya watumishi kutoka 2,698 mwaka 2022 hadi kufikia 3,500 ifikapo mwaka 2025.

ii. Kuongeza Hospitali kutoka 16 mwaka 2022 hadi 18 ifikapo mwaka 2025.
iii. Kuongeza Vituo vya afya kutoka 47 kwa mwaka 2022 hadi 60 ifikapo mwaka 2025.
iv. Kuongeza zahanati kutoka 404 kwa mwaka 2022 hadi 450 ifikapo mwaka 2025.
v. Kuongeza upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 90 ya mwaka 2022 hadi asilimia 100 ifikapo mwaka 2025.
vi. Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka 547 (6/1000) kwa mwaka 2021/2022 hadi vifo 410 mwaka 2025.
vii. Kuongeza asilimia ya wahisiwa wa UKIMWI kufahamu hali zao za maambukizi kutoka asilimia 80 ya mwaka 2021/2022 hadi asilimia 95 ifikapo mwaka 2025.
viii. Kiwango cha ukondefu au utapiamlo mkali kwa watoto wenye umri wa miezi 0-59 kupungua kutoka asilimia 3.7 mwaka 2022 hadi asilimia 1.8 ifikapo mwaka 2025.
ix. Hali ya udumavu au utapiamlo sugu kwa watoto wenye umri wa mwezi 0-59 kupungua kutoa asilimia 37.2 mwaka 2022 hadi asilimia 18.8 ifikapo mwaka 2025.
x. Hali ya uzito upungufu kwa watoto wenye umri wa miezi 0-59 kupungua kutoka asilimia 17.8 mwaka 2022 hadi asilimia 8.9 ifikapo mwaka 2025.

### 3.4 Malengo ya Sekta ya Kilimo

Lengo Kuu ni kuimarisha usalama wa chakula na kuinua kipato cha wananchi wa Mkoa wa Dodoma. Ili kufikia azma hiyo Mkoa umepanga kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kipaumbele ambayo ni Mtama, Uwele, alizeti na zabibu kama ifuatavyo;

i. Mtama na Uwele kutoka tani 0.6 mwaka 2022 hadi tani 1 mwaka 2025
ii. Mpunga kutoka tani 1 mwaka 2022 hadi 1.5 mwaka 2025
iii. Mihogo kutoka tani 3 mwaka 2022 hadi 4 mwaka 2025
iv. Alizeti kutoka tani 0.6 mwaka 2022 hadi tani 1 mwaka 2025
v. Zabibu kutoka tani 1 mwaka 2022 hadi 1.5 mwaka 2025

### 3.5 Malengo ya Sekta ya Mifugo

Pamoja na Mkoa wa Dodoma kuweza kustawisha Mifugo ya aina nyingi, Mkoa umeweka kipaumbele katika kuzalisha mazao ya ng'ombe, mbuzi, Kondoo na kuku. Lengo kuu la mkoa ni kuongeza tija katika uzalishaji wa nyama, maziwa na mayaikufikia viwango vifuatavyo;

i. Nyama ya ngombe: Kutoka kilo 120 mwaka 2022 hadi kilo 150 mwaka 2025
ii. Nyama ya Mbuzi: Kutoka kilo 12 mwaka 2022 hadi kilo 20 mwaka 2025.

iii. Nyama ya Kuku: kutoka kilo 1 mwaka 2022 hadi 1.5 mwaka 2025.
iv. Maziwa ya ng'ombe kutoka lita 2 kwa siku mwaka 2022 hadi lita 10 mwaka 2025.
v. Mayai: kutoka mayai 10 mwaka 2022 hadi 20 kwa kipindi kimoja cha kutaga mwaka 2025

### 3.6 Malengo ya Sekta ya Maliasili na Utalii

Lengo la mkoa wa Dodoma ni ni kuifanya kuwa ya kijani ili kutunza na kupendezesha mandhari kwa manufaa ya viumbe hai vinavyoishi katika mkoa huu. Malengo mahsus ya Sekta ya Maliasili na utalii ni kama ifuatavyo

i. Kila Halmashauri kupanda na kukuza miche 1,500,000 kila mwaka.
ii. Kudhibiti uharibifu wa misitu ya asili.
iii. Kuendeleza utalii wa aina mbalimbali kama historia na mali kale eneo lililotumiwa na wapigania uhuru wa nchi za kusini mwa bara la Afrika lililopo Kongwa mjini, utalii wa zabibu na mazao yake kama mvinyo, utalii wa kutembelea mapori ya akiba ya Mkungunero na Swagaswaga, utalii wa kutembelea mbuga za wanyama zilizo karibu na mkoa wa Dodoma kama Tarangire, Manyara na Ruaha na utalii wa mikutano.

## 3.7 Malengo ya Sekta ya Viwanda

i. Kuongeza uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali

## 3.8 Malengoya Sekta ya Ushirika

i. Kuvifanya vyama vya Ushirika kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kilimo, mifugo, uvuvi na masoko.

## 3.9 Malengo TANROADS mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Kuhakikisha mtandao wa barabara wenye jumla ya Km 1696.68 na madaraja **23** upo katika hali nzuri katika kipindi chote cha mwaka.
ii. Ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa Nje (*Outer Ring Road*) yenye urefu wa km 112.3 unakamilika kabla au ifikapo Machi 2025.
iii. Ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa kati (*Middle Ring Road*) yenye urefu wa km 46 unatekelezwa na kukamilika kama ilivyopangwa.
iv. Ujenzi wa barabara nne zenye urefu wa km 220 katika barabara (Dodoma – Morogoro 70Km, Dodoma – Singida 50Km, Dodoma – Iringa 50Km na Dodoma – Babati 50Km).

## 3.10 Malengo TARURA mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Kuhakikisha mtandao wote wenye km **7314.315** upo katika hali nzuri na unapitika katika kipindi chote cha mwaka ukilinganisha na hali ya sasa ambapo barabara zenye hali nzuri ni km **1670.185,** zenye hali ya wastani ni **2604.893**, na zenye hali mbaya ni **3265.944.**

## 3.11 Lengo Uwanja wa Ndege mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Kuhakikisha Jiji la Dodoma linaungwashwa na majiji mengine kwa kuwepo na uwanja wa ndege wa kisasa unaweza kuhudumia safari za kitaifa na kimataifa.

## 3.12 Malengo Sekta ya Maji mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Huduma ya maji katika miji asilimia 90, katika miji midogo ya Wilaya na asilimia 95 katika Majiji na Miji ya makao makuu ya Wilaya ifikapo 2025.
ii. Kuongeza upatikanaji wa maji kutoka masaa 10 ya sasa hadi kufikia 24.
iii. Kuongeza huduma ya maji taka kutoka 20 ya sasa hadi 45 ifikapo 2025.

## 3.13 Malengo RUWASA mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Kuhakikisha huduma ya maji vijijini inapatika kwa asilimia 85.

## 3.14 Malengo TANESCO mwaka 2022/2023 hadi 2025/26

i. Kuvifikia vitongoji na mitaa 1528 ambavyo kwa sasa havina umeme kati ya 3446 vilivyopo mkoani Dodoma.

## 3.15 Malengo Sekta ya TEHAMA

i. Kuhakikisha rasilimali za TEHAMA kama mifumo, seva na vitendea kazi vingine vinasimamiwa kwa namna ambayo haitaathiri ulinzi, usalama, uadilifu na upatikanaji wa taarifa.
ii. Kuendeleza utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa serikali katika maswala | mifumo ya TEHAMA.
iii. Kushirikiana kwa ukaribu na wataalamu wa TEHAMA kutoka TAMISEMI, Halmashauri, wizara na taasisi nyingine za serikali ili kubadilishana uzoefu na kujengeana uwezo.
iv. Kuendelea kutoa msaada wa kiufundi kwa watumishi ndani ya mkoa wa Dodoma.